# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

FEBRUARI, 2025

## YALIYOMO

*SEHEMU YA KWANZA* 1

UTANGULIZI 1

Muundo wa Kamati ya Bajeti 2

*SEHEMU YA PILI* 4

TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR 4

Ukuaji wa Uchumi 4

Mfumko wa Bei 4

Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania 5

Idadi ya Watalii 6

Changamoto Zilizobainika 7

Maoni na Ushauri wa Kamati 7

*SEHEMU YA TATU* 9

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 9

Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 9

Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025 9

Tathmini ya Mwenendo wa Deni la Taifa 9

Changamoto Zilizobainika 10

Maoni na Ushauri wa Kamati 10

*SEHEMU YA NNE* 10

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 12

Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 12

Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025 13

Changamoto Zilizobainika 13

Maoni na Ushauri wa Kamati 14

Tathmini ya Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi na Programu mbalimbali zilizotembelewa na Kamati ya Bajeti 15

Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali 15

Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais 16

Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) 17

Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Unguja 20

Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Biochemistry 21

Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar 22

Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) Zanzibar 23

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme 25

Mradi wa Uimarishaji Maeneo Huru ya Uwekezaji 26

Mradi wa Kuimarisha Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Park) 28

Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho ya Kimataifa Zanzibar 30

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Big Z) 31

Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) Kipindi cha Pili 33

Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu 34

Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani 35

Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini 36

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya 37
Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya 38
Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda 40
Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Maonesho Dimani Fumba 41
Programu ya Uimarishaji wa Ubora wa Elimu 42
Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (OMKR) 43
Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira 44
Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani 44
Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani 45
Miradi ya Iliyotekelezwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU) 46
Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki 47
Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini 47
Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini 48
Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo 49
Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu, Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani na Programu ya Matengeneo ya Barabara za Mjini 50
Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu Utekelezaji wa Barabara za Tunguu – Makunduchi, Fumba Kisauni na Chake Chake – Mkoani 51
Programu ya Ujenzi Barabara ya Chake – Wete 51
Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani 51
Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini 52
Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar 53
Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Masheha Unguja na Pemba 55
Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM na Mradi wa Uzamiaji na Uwokozi 56
Mradi wa Kijani Pemba (Green & Smart Cities "SASA") 57

*SEHEMU YA TANO* 59

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 59
Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025 60
Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025 60
Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025 63
Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) 64
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar 65
Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) 65
Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) 66
Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) 67
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) 67
Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) 68
Changamoto Zilizobainika 68
Maoni na Ushauri wa Kamati 69

*SEHEMU YA SITA* 72

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA 72
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) 72
Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) 74
Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) 77
Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) 79
Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) 82

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) 84
Shirikia la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) 85
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 86

Maoni na Ushauri wa Jumla 87

*SEHEMU YA SABA* 89

HITIMISHO 89

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Bajeti ni moja ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, iliyoanzishwa kwa Kanuni ya 119(1) ya Kanuni za Baraza, Toleo la 2024. Kamati hii ina jukumu la kusimamia masuala ya bajeti kwa mujibu wa mwongozo uliotajwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizo. Sambamba na hilo, Kamati hii hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba, Sheria, na miongozo mbalimbali ya taifa ili kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali na utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Majukumu ya Kamati ya Bajeti kama yalivyoainishwa katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:

i. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;

ii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

iii. Kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za fedha na sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;

iv. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

v. Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Baraza na Kamati za Kudumu za Baraza;

vi. Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali;

vii. Kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Kudumu za Baraza wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kutoa ushauri na maagizo kwa Serikali;

viii. Kuchambua mapendekezo ya jumla ya Serikali kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi;

ix. Kufikiria na kuchunguza Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa na Spika;

x. Kuchambua mapendekezo ya Serikali endapo itataka kuwasilisha katika

Baraza Mswada wa Matumizi ya Nyongeza kwa mujibu wa kanuni ya 114 ya Kanuni hizi;

xi. Kufuatilia namna sheria zilizotungwa na Baraza zinavyotekelezwa na kujua changamoto za sheria hizo; na

xii. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia na kutathmini taarifa ya Wizara juu ya utekelezaji wa maagizo hayo na kuwasilisha katika Baraza maoni ya Kamati kuhusu taarifa hiyo.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya vikao pamoja na Mawaziri na Watendaji mbalimbali wa Wizara, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tawala za Mikoa, Idara Maalum za SMZ. Aidha, Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kukagua miradi ya maendeleo. Lengo kuu la vikao hivyo lilikuwa kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za taasisi zao na kutoa maoni na ushauri utakaosaidia kuimarisha utendaji kazi wa taasisi hizo.

**Muundo wa Kamati ya Bajeti**

Kamati ya Bajeti inajumuisha Wajumbe nane (8) na Makatibu Kamati wanne (4) kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Abass Vuai Mohammed | Katibu |
| 11. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 12. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

Msingi wa ripoti hii ya Kamati ya Bajeti ni matakwa ya Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Baraza, Toleo la 2024 ambayo inaitaka Kamati kuwasilisha Ripoti ya shughuli zake

mbele ya Baraza katika Mkutano wa mwezi Februari au wakati mwengine utakaoamuliwa na Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza.

Ripoti ya Kamati ya Bajeti imegawanywa katika sehemu saba (7). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi; **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024; **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025; **Sehemu ya Nne** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025; **Sehemu ya Tano** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025; **Sehemu ya Sita** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma; na **Sehemu ya Saba** ni Hitimisho.

# SEHEMU YA PILI

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2024

Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar unategemea kwa kiasi kikubwa na hali ya viashiria vya uchumi kama vile ukuaji wa uchumi, mfumko wa bei, mwenendo wa sarafu ya Tanzania, pamoja na idadi ya watalii waliyoingia Zanzibar.

## Ukuaji wa Uchumi

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2024/2025, hali ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar imeendelea kuwa ya kuridhisha ambapo hadi kufikia mwezi wa Septemba mwaka 2024 kasi ya ukuaji uchumi wa Zanzibar imeendelea kuimarika na kufikia asilimia 7.5 kutoka wastani wa asilimia 7.4 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii, kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuimarika kwa huduma za malazi na chakula, na kuimarika kwa biashara.

## Mfumko wa Bei

Mwaka 2024, mfumko wa bei wa Zanzibar ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumko wa bei na kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja kulichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko yetu. Mfumko huu wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja kutokana na utulivu wa thamani ya Shilingi. Jadweli Nam. 1 linafafanua.

**Jadweli Nam. 1: Mfumko wa Bei kwa kila mwezi kwa mwaka 2023 na 2024**

| Mwezi | Mfumko wa Bei (Asilimia) | |
|---|---|---|
| | 2023 | 2024 |
| Januari | 8.4 | 5.3 |
| Februari | 7.8 | 5.1 |
| Machi | 7.1 | 4.9 |
| Aprili | 7.5 | 4.9 |
| Mei | 6.4 | 5.3 |
| Juni | 6.5 | 5.7 |
| Julai | 6.7 | 5.3 |

| | | |
|---|---|---|
| Agosti | 6.8 | 5.1 |
| Septemba | 7.5 | 4.8 |
| Oktoba | 6.5 | 5.8 |
| Novemba | 6.3 | 4.5 |
| Disemba | 5.5 | 4.9 |
| **Wastani kwa Mwaka** | **6.9** | **5.1** |

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2024)

## Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania

Mwaka 2024, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani iliendelea kuwa tulivu licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika uchumi wa dunia. Katika kipindi cha Julai - Disemba mwaka 2024, Shilingi ya Tanzania imeshuka thamani dhidi ya Dola ya Kimarekani kwa wastani wa asilimia 7.8 kufikia thamani ya TZS 2,647.12 kwa USD 1 ikilinganishwa na wastani wa thamani ya TZS 2,451.1 kwa USD 1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Kupungua kwa thamani ya shilingi kulichangiwa na hatua zilizochukuliwa na nchi zilizoendelea katika kukabiliana na mfumko wa bei ikiwemo utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ujazo wa fedha. Kamati inaipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa kuendelea kuchukua hatua za kuiweka Sarafu ya Tanzania katika hali ya utulivu ili kuongeza mzunguko wa fedha ikiwemo kuweka udhibiti wa riba za benki za kibiashara.

## Uingiaji wa Watalii

Mwaka 2024, idadi ya watalii walioingia Zanzibar imeongezeka na kufikia watalii 736,755 ikilinganishwa na idadi ya watalii 638,498 kwa mwaka 2023 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko hili ni wageni kuvutika na hali ya kuongezeka kwa hoteli za kitalii zenye hadhi ya juu pamoja na jitihada za Serikali kutangaza utalii kupitia maonesho ya kimataifa na ya kikanda, na pia kupitia matamasha, makongamano na warsha za kimataifa.

**Jadweli Nam. 2: Idadi ya Watalii kwa kila mwezi kwa mwaka 2023 na 2024**

| Mwezi | Idadi ya Watalii |
|---|---|

| | 2023 | 2024 |
|---|---|---|
| Januari | 68,813 | 73,468 |
| Februari | 65,430 | 71,095 |
| Machi | 45,915 | 51,879 |
| Aprili | 27,666 | 28,995 |
| Mei | 26,620 | 29,995 |
| Juni | 47,595 | 51,559 |
| Julai | 58,711 | 68,223 |
| Agosti | 61,466 | 72,296 |
| Septemba | 53,839 | 60,731 |
| Oktoba | 54,961 | 69,860 |
| Novemba | 57,296 | 67,049 |
| Disemba | 70,186 | 91,611 |
| **Jumla** | **638,498** | **736,755** |

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2024)

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa upungufu wa uzalishaji wa ndani hali inayopelekea Zanzibar kuwa tegemezi wa uagizaji wa bidhaa hususan kwa zile bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa katika nchi yetu. Mathalan, Zanzibar bado inaagiza mboga mboga kama vile tungule, pilipili na keroti, pia tunaagiza vitoweo kama vile samaki na kuku ambao tunaweza kuzalisha hapa hapa nchini.
ii. Kuwepo kwa uhaba wa ajira na ujuzi wa kazi, hasa kwa vijana. Hali hii husababisha kuongezeka kwa changamoto za kiuchumi na kijamii.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali, kuendelea na juhudi madhubuti za kuzalisha ajira sambamba na kuimarisha mfumo wa mafunzo ya amali ili kuzalisha wahitimu wenye ujuzi na sio kubobea katika nadharia tu.
ii. Ili kuongeza fursa za ajira na kuinua uchumi wa wananchi, Serikali inapaswa kuimarisha sekta zinazojumuisha idadi kubwa ya watu, kama vile kilimo na

uvuvi. Hatua hii inaweza kufanikishwa kwa kuimarisha miundombinu ya kilimo, kama vile upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya kilimo, mbegu bora, pembejeo na teknolojia za kisasa, pamoja na kuweka mifumo bora ya masoko ili kuhakikisha wakulima wanapata faida stahiki. Vilevile, sekta ya uvuvi inaweza kuimarishwa kwa kuwekeza katika vifaa vya kisasa vya uvuvi, kutoa mafunzo kwa wavuvi na kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi na kusindika mazao ya uvuvi. Kupitia juhudi hizi, Serikali itaweza kuongeza uzalishaji, kuinua kipato cha wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi.

iii. Ukifanya uchambuzi kwa wageni waliyofika Zanzibar kwa mwaka 2024, utagundua asilimia 72 wanatoka nchi za Ulaya, asilimia 7 kutoka nchi za Asia, asilimia 13 kutoka nchi za Afrika na asilimia 8 kutoka nchi za Australia na Oshania. Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada na mikakati ya kuendelea kuutangaza utalii hususan katika nchi za Asia kama vile China, India, Falme za Kiarabu badala ya kutegemea zaidi watalii wanaotoka bara la Ulaya.

iv. Kamati inaishauri Serikali, kuendelea kuwasaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kuwawezesha kupata mikopo na mafunzo.

## SEHEMU YA TATU

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imekusanya jumla ya TZS 2,770.46 bilioni sawa na asilimia 97.52 ya makadirio ya TZS 2,840.85 bilioni. Mapato hayo yanajumuisha TZS 1,424.42 bilioni ya mapato ya ndani, TZS 13.27 bilioni Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na TZS 639.65 bilioni ni mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilitumia jumla ya TZS 2,640.16 bilioni sawa na asilimia 92.94 ya makadirio ya TZS 2,840.85 bilioni. Matumizi hayo yanajumuisha TZS 1,219.79 bilioni zilizotumika kwa kazi za kawaida na TZS 1,407.10 bilioni kwa kazi za Maendeleo. Aidha, matumizi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa TZS 13.27 bilioni.

### Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Serikali ilikadiria kukusanya TZS 1,456.62 bilioni ambapo mapato halisi yamefikia TZS 1,405.45 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya mapato hayo, Mapato ya ndani ni TZS 958.27 bilioni, Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni TZS 6.16 bilioni na

Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 163.03 bilioni.

Kwa upande wa matumizi katika kipindi hicho, Serikali ilitumia kiasi TZS 1,659.93 bilioni zimetumika sawa na asilimia 103.79 ya makadirio ya kutumia TZS 1,599.39 bilioni. Matumizi haya pia yanajumuisha TZS 6.94 bilioni kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na TZS 72.68 bilioni kutoka Taasisi zinazojitegemea. Jumla ya TZS 832.06 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 827.86 bilioni zilitumika kwa kazi za Maendeleo.

### Tathmini ya Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa la Zanzibar limegawika katika sehemu mbili, Deni linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Deni linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT). Hadi kufikia Disemba 2024, Deni la Zanzibar limefikia TZS 1,246.99 bilioni ikilinganishwa na TZS 870.3 bilioni mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 43.3. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni inaonesha Deni la Zanzibar bado ni himilivu.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuendelea kubadilika kwa miundo ya baadhi ya taasisi za umma kutokana na mabadiliko ya sheria ambapo inasababisha kuongezeka kwa fungu la mishahara na maslahi yao na hivyo kusababisha kuongezeka kwa matumizi ya bajeti ya mishahara.
ii. Malipo ya madeni mbali mbali ambayo hayakuzingatiwa katika bajeti wakati wa matayarisho.
iii. Kujitokeza kwa mahitaji ya dharura.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na hatua za usimamizi wa matumizi ya fedha ikiwemo kuimarisha zaidi taratibu za ndani za matumizi pamoja na mifumo ya kidijitali ya usimamizi.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali ikiwemo kushajihisha mashirikiano na sekta binfasi katika utaratibu wa EPC+F.
iii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kupitia miongozo ya utoaji misamaha kwa lengo la kuendelea kupunguza misamaha isiyokuwa na maslahi kwa nchi yetu.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuanza utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma sambamba na kutunga kanuni zake kwa haraka ili lengo la kupunguza muda, kuongeza ufanisi pamoja na kuimarisha usimamizi na thamani ya fedha katika mchakato wa ununuzi wa umma. Hatua hii itasaidia sana kuimarisha matumizi ya fedha za umma.
v. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha taasisi zake zinazosimamia ukusanyaji wa kodi na kuimarisha utendaji wake sambamba na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi.
vi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kushajihisha wananchi katika ulipaji wa kodi kwa hiari, kutoa na kudai risiti.
vii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na usimamizi wa matumizi ya Serikali kwa kuimarisha zaidi taasisi zinazosimamia uwajibikaji ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.
viii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwani ni muhimu sana ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinatumika kwa ufanisi, uwazi, na kwa manufaa ya wananchi wote. Hatua hii inaweza kufikiwa kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuimarisha ukaguzi wa ndani ili kuhakikisha fedha zote zinatumika kama ilivyopangwa, na kutathmini ufanisi wa matumizi ya Serikali kwa kuangalia athari zake kwa maendeleo ya wananchi badala ya kuangalia tu kiasi cha fedha kilichotumika.
ix. Kamati inaishauri Serikali kuvipitia vyanzo vyote vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa Unguja na Pemba, na kuvifanyia tathmini ya mwenendo wa ukusanyaji mapato. Baada ya hapo Serikali iweke malengo ya mapato kila chanzo na kwa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali ihakikishe makusanyo yote yanapitia katika mifumo ya kielektroniki iliyounganishwa na ZanMalipo. Hatua hii itasaidia kuepusha uvujaji wa mapato ya Mamlaka hizo.

# SEHEMU YA NNE

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mipango ya Maendeleo kwa kila mwaka kuanzia mwaka 2020/2021 mpaka mwaka 2025/2026 ni mwendelezo wa kutekeleza mikakati iliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 (Vision 2050), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021 – 2025 (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 na maelekezo na miongozo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Kumi la Wawakilishi mwezi Novemba 2020.

### Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

Mpango wa Maendeleo wa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni utekelezaji wa Mpango wa Tatu Maendeleo wa Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) 2020/2021 - 2025/2026. Mpango huu wa Maendeleo ulilenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi kwa kuimarisha uchumi wa buluu, miundombinu, huduma za kijamii, pamoja na utawala bora na uhimilivu. Maeneo haya yamewekwa kwa matarajio ya kuleta matokeo makubwa na kwa haraka ikiwemo kuongeza mapato ya Serikali, upatikanaji wa ajira za ziada kwa wananchi, uwekezaji pamoja na kuimarisha hali za wananchi. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi 16 ya kimkakati ilipewa kipaumbele na kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka ea fedha 2023/2024.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya TZS 915.87 bilioni zilipangwa kutumika ili kutekeleza programu na miradi ya kimkakati ambapo matumizi halisi yalikuwa TZS 856.57 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TZS 465.86 bilioni sawa na asilimia 94 ya lengo la TZS 495.58 bilioni zilipatikana kutoka Serikalini na TZS 425.98 bilioni sawa na asilimia 101 ya lengo la TZS 419.97 bilioni zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) 2020/21 - 2025/2026 umeendelea kutekelezwa kwa mwaka wa nne kupitia utekezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2024/2025. Serikali inaendelea kugharamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile Kuimarisha Uchumi wa Buluu, Kuimarisha Miundombinu, Kufanya Mageuzi ya kiuchumi, Kuimarisha Huduma za Kijamii; pamoja na Kuimarisha Utawala Bora. Maeneo haya yamewekwa kwa matarajio ya kuleta matokeo chanya na kwa haraka zaidi. Utekelezaji wa maeneo haya utaongeza mapato ya Serikali, upatikanaji wa ajira kwa wananchi, utaimarisha uwekezaji, utaimarisha ubora wa mazingira ya kufanyia kazi pamoja na kuimarisha hali za wananchi. Kupitia utekelezaji wa maeneo hayo, programu na miradi 23 imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya TZS 2,086.72 bilioni zimepangwa kutumika ili kutekeleza programu na miradi ya kimkakati. Aidha, katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, jumla ya TZS 388.6 bilioni sawa na asilimia 38 ya lengo la TZS 1,027.4 bilioni zimepatikana. Kati ya fedha hizo, TZS 352.7 bilioni ni kutoka Serikalini sawa na asilimia 67 ya lengo na TZS 35.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 7 ya lengo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa kuanza utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa muda mrefu, hali ambayo inapelekea kuanza kwa malipo ya riba kabla ya mradi kuanza au kukamilika. Kwa mfano, Katika Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia ufadhili wa BADEA, mradi umesainiwa mwaka 2012, ujenzi haukuanza hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni, 2024.
ii. Kuchelewa kuanza kwa taratibu za ununuzi ambazo zimeathiri baadhi ya shughuli zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa mfano kwenye Sekta ya Afya, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi ulitegemewa kumalizika katika kipindi cha miezi 12 lakini ulianza katika robo ya tatu (3) ya mwaka wa fedha 2023/2024.
iii. Kuongezeka kwa mawanda ya kazi (Variation) kutoka bajeti ya awali katika baadhi ya Miradi ya Ujenzi wa Skuli kama vile Ujenzi wa Skuli ya Mfenesini na Gamba.
iv. Kuchelewa kutolewa kwa wakati vifaa kutoka bandarini kwa baadhi ya miradi. Mathalan, mradi ambao umeathirika zaidi na changamoto hii ni Mradi wa Maji

ambao unatekelezwa kwa fedha kutoka Benki ya EXIM ya India.

v. Kuchelewa kupatikana kwa wakati kwa fedha za mikopo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

vi. Kuchelewa kupatikana kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kutokana na mabadiliko ya Sera za nchi husika.

vii. Baadhi ya watendaji kuwa na uwezo mdogo wa usimamizi wa miradi hususan katika eneo la ununuzi ambapo inapelekea kuchelewa kuanza kwa baadhi ya shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan miradi inayotekelezwa kwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mfano, Mradi wa Kijani Pemba.

viii. Kuwepo kwa baadhi ya watendaji kutozingatia mahitaji ya miradi katika hatua za awali jambo ambalo husababisha ongezeko la fedha za miradi hiyo.

ix. Kujitokeza kwa madai mbali mbali ya fidia kutoka katika maeneo ya ujenzi wa miradi ya miundombinu ambapo baadhi ya madai hayaakisi thamani halisi ya maeneo husika.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inajiandaa vyema kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili inaposainiwa mikataba na kuingizwa kwa fedha za miradi iweze kutekeleza miradi hiyo bila ya kuchelewa ili Serikali isipoteze fedha nyingi kwa ajili ya malipo ya riba.

ii. Kamati inashauri Serikali kuepuka kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja na badala yake kuweka kipaumbele kwenye miradi inayoweza kutekelezwa kwa ufanisi ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Hii inaweza kufanikiwa kwa kuhakikisha miradi inayoendelea inakamilika kwanza kabla ya kuanzisha mipya, hivyo kuepuka mgawanyo wa rasilimali chache tulizonazo katika maeneo mengi na hatimae kushindwa kuikamilisha kwa wakati hali inayochelewesha maendeleo na kuingiza hasara.

iii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ihakikishe inawapatia Maafisa Masuuli maelekezo maalum ya namna ya kufuata taratibu za miradi husika ili kuhakikisha wanaanza mapema mchakato wa ununuzi na kuepusha uchelewaji wa kuanza kwa miradi hiyo. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe inaifuatilia miradi yote na kubaini changamoto na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka ili kuepusha mkwamo wa miradi.

iv. Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar ihakikishe upembuzi yakinifu wa miradi unafanyika mapema zaidi ili kupatiwa bajeti inayostahiki kwa mradi kutekelezeka bila ya mikwamo yoyote.
v. Kamati inaishauri Serikali kuwashirikisha wananchi mapema kabla ya kuanza kutekeleza miradi. Hatua hii itasaidia kuongeza ufahamu wa miradi husika na hatimae kupunguza ukaidi wa kupisha katika maeneo iliyopangwa kutekelezwa miradi hiyo. Kwa sasa taasisi nyingi za umma hufanya mawasiliano na viongozi tu katika maeneo ya inayotekelezwa miradi kama vile Wakuu wa Mikoa na Wilaya, pamoja na Masheha na sio wananchi.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi na Programu Mbalimbali zilizotembelewa na Kamati ya Bajeti

### Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali

Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali unatekelezwa na Afisi ya Rais – Ikulu (ARI) na una lengo la Kufanya Matengenezo ya Ikulu na Ikulu Ndogo (States Lodges).

Katika wa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa TZS. 2.4 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024, ulishaingiziwa TZS 600 milioni ambazo ni sawa na asilimia 25 ya fedha zilizopangwa. Aidha, kiasi cha fedha kilichotumika kwa kipindi hicho ni TZS 412.325 milioni ambazo ni sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoingizwa. Fedha hizo zimetumika kufanya matengenezo ya ukumbi mkubwa wa kuapishia viongozi katika jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja, matengenezo ya dharura katika Ikulu ndogo ya Dar es Salaam (Liabon) na Migombani ambayo yalikuwa yanaendelea kipindi Kamati ya Bajeti ilipofanya ziara.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali **kuimarisha Mpango wa Bajeti na Upangaji wa Vipaumbele.** Kuandaa bajeti yenye uhalisia na kuweka kipaumbele kwa miradi

muhimu kama hii ya Afisi ya Rais – Ikulu (ARI) ambayo itasaidia kuimarisha Ikulu na Ikulu Ndogo (States Lodges).

ii. Kwa kuwa Ikulu ndogo ya Wete imekabidhiwa kwa Serikali ya Muuungano wa Tanzania (SMT), Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Ikulu (ARI) kufanya mawasiliano na SMT na kuiomba kufanya marekebisho au kuijenga upya ili kuiweka katika hali nzuri kwani kwa sasa, mazingira ya Ikulu hiyo hayapo vizuri. Ikiwa hatua za hizo zitashindikana, Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Ikulu kuiomba SMT kuirudishia ili iweze kuifanyia matengenezo au kuchukua hatua nyengine zitakazoonekana zinafaa.

### Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais

Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais unatekelezwa na Afisi ya Rais – Ikulu (ARI). Mradi huu umeendelea kwa Awamu ya Pili katika mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo umeanza mwaka wa fedha 2022/2023. Lengo la mradi huu ni kuimarisha Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Maakazi ya Mheshimiwa Rais.

Katika wa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa TZS 1.0 bilioni ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024, kiasi cha fedha kilichoingizwa ni TZS 248.070 milioni sawa na asilimia 24.80 ya fedha zilizopangwa. Aidha, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 fedha zilizotumika ni TZS 72.848 milioni ambazo ni sawa na asilimia 29.4 ya fedha zilizopatikana. Kazi zilizofanyika kwa kipindi hicho ni pamoja na kuweka mfumo wa CCTV katika Ikulu Ndogo ya Pagali, na kufanya masawazisho ya uwekaji wa kamera katika Ikulu ya Mnazi Mmoja.

#### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa uhaba wa fedha kwa ajili ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

#### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali **kuimarisha Mpango wa Bajeti na Upangaji wa Vipaumbele.** Kuandaa bajeti yenye uhalisia na kuweka kipaumbele kwa miradi muhimu kama hii ya Afisi ya Rais – Ikulu (ARI) ambayo itasaidia kuimarisha Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Maakazi ya Mheshimiwa

Rais.

## Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET)

Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation - HEET) unatekelezwa Tanzania nzima na una thamani ya USD 425 milioni sawa na TZS 972 bilioni ambazo ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB).

Kwa upande wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ndio kilichonufaika na mradi huu, kikiwa ni moja katika vyuo vikuu 14 vya Tanzania.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimetengewa jumla ya USD 20 milioni sawa na TZS 45.9 bilioni. Mradi huu ambao umeanza kutekelezwa mwaka 2023, unatarajiwa kukamilika mwaka 2027.

Kupitia mradi huu wa HEET, SUZA inatekeleza maeneo manne (4) kama ifuatavyo:

i. Eneo la ujenzi au ukarabati wa miundombinu (Construction or rehabilitation of infrastructure) Eneo hili la SUZA (Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar) limetengewa USD 14.849 milioni sawa na TZS 38.228 bilioni, ambapo hadi Oktoba 2024, asilimia 3.8 tu (USD 564,277) zimetumika. Fedha hizo zimetumika kwa ujenzi wa miundombinu (maabara ya sayansi na skuli ya kilimo Tunguu) ambapo zimetumika USD 331,625 sawa na TZS 699.514 milioni na uimarishaji wa vifaa vya kujifunzia ununuzi wa vifaa vya TEHAMA, vifaa vya wenye mahitaji maalum, pamoja na kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo zimetumika USD 40,629 sawa na TZS 104.597 milioni. Ujenzi mkubwa unatarajiwa kuanza Novemba 2024 na kukamilika Juni 2026.

ii. Eneo la uimarishaji wa mitaala na kuanzisha mbinu bora za ufundishaji (Updating curriculum and introducing innovative pedagogical methodologies). Eneo hili limetengewa jumla ya USD 430,000 sawa na TZS 1.107 bilioni kwa ajili ya uimarishaji wa mitaala nane (8) iliyopo na utayarishaji wa mitaala mipya tisa (9). Eneo hili pia linatekelezwa sambamba na eneo la Uhusiano wa Kitasnia (Building Functional Linkages with Private Sector/Industry). Hadi kufikia Oktoba 2024, jumla ya USD 291,225 sawa na TZS 749.741 milioni

ambazo ni wastani wa asilimia 68 ya bajeti zimetumika.

iii. Eneo la kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kufundisha na kujifunza (Strengthening use of digital technology). Eneo hili limetengewa jumla ya USD 332,033 sawa na TZS 854.799 milioni kwa ajili ya uanzishwaji wa mfumo wa kujifunza na kufundishia kwa njia ya kidijitali (LMS Moodle), kuweka miundombinu ya kisasa ya TEHAMA na kuwajengea uwezo wanataaluma na wataalamu wa TEHAMA, kuandaa maudhui ya kujifunzia na kufundishia kwa njia ya kidijitali na kuwapatia mbinu bora za ufundishaji kwa njia ya mtandao (Open and Distance Learning (ODL). Hadi kufikia Oktoba 2024 jumla ya USD 78,516 sawa na TZS 202.134 milioni ambazo ni wastani wa asilimia 24 ya bajeti zimetumika.

iv. Eneo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kitaaluma na Uongozi wa Chuo Kikuu (Building capacity of academic staff and university leadership). Eneo hili linahusika kuwajengea uwezo wanataaluma 70 (30 kwa ngazi ya PhD na 40 Master) pamoja na kuwapatia mafunzo mafupi wafanyakazi wengine 50 wa kada ya ufundi, utawala na uongozi ili kuwaongezea ujuzi na maarifa katika kufanya kazi zao, kutengeneza na kununua mifumo (13) ya Chuo kama vile mfumo wa udahili na mitihani (SUZIMS), Mfumo wa usimamizi wa fedha na shughuli nyengine za kiutawala (ERMS), ununuzi wa samani za ofisi na vifaa vya kiofisi, gari mbili za mradi na kuwajengea uwezo watendaji wa mradi. Eneo hili pia linahusika na uwezeshaji wa Ofisi ya uratibu wa mradi. Jumla ya USD 3.340 milioni sawa na TZS 8.598 bilioni zimetengwa ambapo hadi kufikia Oktoba 2024 jumla ya USD 1.750 milioni sawa na TZS 4.505 bilioni zimetumika.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mradi una mahitaji makubwa ya muda, rasilimali watu na fedha ambazo hazikupangwa katika bajeti kutokana na masharti ya utekelezaji yaliyowekwa;
ii. Taratibu za ununuzi zinapelekea kuchelewa kwa upatikanaji wa bidhaa ya huduma na vifaa kunakocheleweshea kwenda kwa kasi ya mradi;
iii. Ujuzi mdogo wa watendaji wa mradi katika utekelezaji wa kazi zake kufuatana na matakwa ya Benki ya Dunia (WB) kuhusiana na utekelezaji wa miradi iliyoifadhili;

iv. Ukosefu wa bajeti kwa baadhi ya vipaumbele vya mradi kunazuia utekelezaji wa kazi zake kwa ufanisi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha SUZA kutenga bajeti maalum ya ndani kwa ajili ya kulipa posho za watendaji wanaotekeleza mradi huu na pia kuweza kutekeleza shughuli zote za mradi ambazo hazitumii fedha za mradi kutoka Benki ya Dunia (WB). Hatua hii itasaidia mradi kutekelezwa kwa haraka na kumalizika ndani ya muda uliyopangwa.

ii. Kamati inaishauri Serikali kutoa msaada wa karibu kwa SUZA katika mradi huu ambao inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) kutokana na SUZA kutokuwa na uzoefu wa miradi ya namna hii. Katika hili, Serikali inaweza kuchagua maafisa wake na kuwaunganisha na timu ya SUZA inayosimamia utekelezaji wa mradi.

iii. Kamati inaishauri SUZA iombe kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kutumia utaratibu maalum wa ununuzi ili iweze kufanikisha ununuzi wa bidhaa na huduma zinazohitajika katika mradi kwa haraka na wakati.

### Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Unguja

Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Unguja unalenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi dawa na vifaa tiba. Bohari zilizopo Maruhubi na Vitongoji zina uwezo mdogo wa kuhifadhi dawa, na hivyo kuna haja ya kujenga bohari mpya yenye uwezo mkubwa zaidi. Mradi huu unafanyika katika eneo la Dunga Zuze - Unguja, na unatarajiwa kusaidia kuimarisha usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya Zanzibar.

Jumla ya fedha za mradi ni TZS 5.23 bilioni. Kati ya hiyo, TZS 500 milioni imetumika hadi sasa kwa malipo ya fidia na ujenzi wa kibanda cha walinzi. Hii inawakilisha takriban asilimia 10 ya utekelezaji wa mradi.

Bado hakuna mkandarasi aliyeteuliwa rasmi kwa ajili ya ujenzi wa bohari, kwani mradi bado uko katika hatua za awali za utekelezaji. Mshauri elekezi ameshafanya Makadirio ya Gharama za Ujenzi (BOQ) na michoro ya ujenzi bila gharama.

Mradi ulianza katika mwaka wa fedha 2023/2024 na unatarajiwa kumalizika katika

mwaka wa fedha 2024/2025, ikiwa fedha za ziada zitapatikana kwa wakati.

Kati ya fedha zilizotumika, TZS 71.2 milioni imetumika kwa malipo ya fidia kwa wakazi wa eneo la ujenzi, na TZS 10.091 milioni zimetumika kwa ujenzi wa kibanda cha walinzi. Fedha zilizobaki, TZS 418,709 milioni zimehaulishwa na kupelekwa katika Mradi wa Ujenzi wa Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU) ktika Hospitali ya Abdalla Mzee. Hatua hii imetokana na kiasi hicho kilichobaki hakikutosha kutumika kwa hatua za ujenzi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kuwepo kwa uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri Serikali kuweka kipaumbele kwenye miradi michache inayoweza kutekelezeka badala ya kuanzisha mingi kwa wakati mmoja hali inayopelekea miradi mingi kutokukamilika kwa wakati.

**Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Biochemistry**

Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Biochemistry unalenga kuimarisha miundombinu ya utafiti wa afya katika Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI). Maabara hii itasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za afya zenye ubora na kukuza utafiti wa magonjwa mbalimbali. Mradi huu unafanyika katika eneo la Binguni na unatarajiwa kuwa na faida kubwa kwa sekta ya afya Zanzibar.

Mradi huu unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 7.2 bilioni. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, zimetengwa TZS 400 milioni kwa ajili ya mradi huu. Fedha ambazo zimeshatumika ni TZS 413.897 milioni ambazo zinafanya takriban asilimia 5.75 ya utekelezaji wa mradi. Mkandarasi (TIL Construction) amefanya kazi za awali kama vile upimaji wa eneo, kuweka uzio, na uvunjaji wa majengo ya zamani ambapo amelipwa TZS 413.897 milioni. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, Wizara ya Afya ilitaka Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) kuvunja mkataba na mkandarasi.

Mradi ulianza katika mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, kutokana na changamoto za kifedha na kuvunjwa kwa mkataba na mkandarasi, haijabainishwa wakati maalum wa kumalizika kwa mradi huu.

**Changamoto Ziliobainika**

i. Kuwepo kwa uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inafanya upembuzi yakinifu wa uhakika kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ili kuepuka kuchelewesha utekelezaji huo. Pia, ni muhimu kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayoendelea kwa kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyostahili.

**Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar**

Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar unatekelezwa na Wizara ya Afya (WA). Mradi huu unalenga kupunguza maambukizi ya malaria na kuimarisha udhibiti wa ugonjwa huo kwa kutumia mikakati mbalimbali kama vile Ufuatiliaji wa Mwenendo na Udhibiti wa Maradhi, Udhibiti wa Mbu wanaoeneza Malaria, Uchunguzi wa Vinasaba vya Mbu. wanaoeneza Malaria, Uchunguzi na Matibabu ya Wagonjwa wa Malaria, Uhamasishaji wa Jamii na Usambazaji wa Vyandarua.

Kwa kipindi cha Januari - Machi 2024, Mradi ulifanikiwa kuingiziwa fedha kwa asilimia 100 ambapo ilikadiriwa kupatikana TZS 800.695 milioni. Hii inaonyesha kuwa shughuli nyingi zilizopangwa zilitekelezwa kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na upigaji dawa katika nyumba, ugawaji wa vyandarua na uchunguzi wa wagonjwa wa malaria.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kuwepo utegemezi mkubwa kwa washirika wa maendeleo katika kutekeleza mikakati ya kumaliza malaria.
ii. Kuwepo ushiriki mdogo wa wadau mbalimbali katika mikakati ya kumaliza malaria.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kushirikisha sekta zisizo za afya katika jitihada za kumaliza malaria.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuanza kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia programu za udhibiti wa magonjwa katika nchi yetu ikiwemo ugonjwa wa malaria.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika tafiti za ndani na uvumbuzi wa mbinu za kudhibiti malaria ili kupunguza utegemezi wa misaada ya nje. Katika hili Serikali inapaswa kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) ili iweze kufanya tafiti kuhusu usugu wa mbu dhidi ya dawa, njia mpya za kudhibiti mazalia ya mbu, na ufanisi wa mikakati ya sasa ya kupambana na malaria.

**Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) Zanzibar**

Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) Zanzibar unatekelezwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU) kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Mradi huu unalenga kuimarisha uzalishaji wa mazao ya baharini, kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, na kukuza mifumo endelevu ya kujikimu. Mradi huu unajikita katika maeneo makuu kama vile miundombinu, masoko, na mafunzo kwa wavuvi na wakulima wa mwani. Lengo kuu ni kushirikisha wanawake na vijana katika shughuli za uvuvi na ufugaji wa viumbe bahari, pamoja na kuimarisha usalama wa chakula na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Jumla ya fedha za mradi ni TZS 5.23 bilioni, ambazo zinatokana na mchango wa IFAD na Serikali ya Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya TZS 500,120,245.16 imetumika, ambayo inawakilisha asilimia 7.5% ya bajeti iliyopangwa. Fedha hizi zimetumika kwa shughuli mbalimbali kama vile ununuzi wa meli ya uvuvi, ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki, mafunzo kwa wavuvi na wakulima wa mwani.

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, mradi umefanikisha kutekeleza asilimia 7.5% ya malengo yake. Hii inaonyesha kuwa shughuli nyingi zilizopangwa bado ziko katika hatua za awali za utekelezaji. Baadhi ya shughuli zilizofanikiwa kuanza ni pamoja na utafiti wa uzalishaji wa samaki, ujenzi wa mitambo ya kukaushia mwani, na mafunzo kwa wakulima wa mwani. Hata hivyo, kuna changamoto zinazohitaji kutatuliwa ili kuhakikisha kuwa mradi unaendelea kwa ufanisi.

Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali kama vile Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO), Taasisi ya Utafiti wa Maliasili za Bahari (ZAFIRI), na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi. Mshauri elekezi wa mradi ni IFAD, ambayo inatoa msaada wa kifedha na kiufundi. Mkandarasi wa shughuli za ujenzi na ununuzi bado

hajateuliwa kwa shughuli nyingi, kwani mradi bado uko katika hatua za awali za utekelezaji.

Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi ulianza rasmi mwaka 2023 na unatarajiwa kuendelea hadi mwaka 2029. Hata hivyo, shughuli za utekelezaji zimekuwa zikiendelea kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, na zinaendelea kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025. Mradi unatarajiwa kukamilika kwa wakati ikiwa fedha za ziada zitapatikana na changamoto za utekelezaji zitashughulikiwa.

Jumla ya fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni TZS 6.696 bilioni. Hadi kufikia Machi 2024/2025, fedha zilizotumika ni TZS 500.12 milioni ambazo ni sawa na asilimia 7.5 ya bajeti iliyopangwa.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo ucheleweshaji katika mchakato wa ununuzi.
ii. Kuwepo ucheleweshaji wa kupata ridhaa (No Objection) kutoka kwa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD).

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU) kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) na kuomba kusaidiwa kupatiwa ufafanuzi wa taratibu za ununuzi za kawaida na za dharura. Hatua hii itasaidia mchakato mzima wa ununuzi kwenda kwa haraka na kukamilika kwa wakati. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ununuzi iratibu mafunzo kwa wafanyakazi wanaoshughulikia manunuzi kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao.

### Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme

Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imetekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme Zanzibar uliyofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya kifalme ya Norway uliosainiwa Disemba 2012 wenye thamani ya USD 212,000. Utekelezaji wa mradi huo ulianza rasmi 2014 na ulitarajiwa kukamilika 2018 lakini kutokana na kutokukamilika kwa wakati kwa baadhi ya taratibu za manunuzi mradi uliweza

kukamilishwa mwaka 2023.

Miongoni mwa kazi zilizofanywa kupitia mradi huu ni pamoja na matengenezo ya laini kubwa za umeme zenye Mkondo wa 33kv kwa baadhi ya maeneo ikiwemo eneo la Pandani hadi Masipa na Pujini hadi Kichaka, kubadilisha mfumo wa miundombinu ya umeme kutoka 11kv hadi 33kv, kufanya marekebisho kwa baadhi ya laini ndogo za umeme pamoja na upelekaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua katika visiwa cha Kokota na Njau.

Mradi umesaidia kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa uhakika kwa wananchi na kuleta ufanisi katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, umepunguza changamoto ya kukatika kwa umeme na umeleta ufanisi katika usimamizi wa matumizi ya umeme na kuondosha malalamiko yanayohusiana na usomaji usio sahihi wa mita za umeme kutokana na kubadilishwa kwa mita za zamani zilizopitwa na wakati.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kutokukamilika kwa wakati kwa taratibu za manunuzi kulirudisha nyuma ununuzi wa vifaa vya mradi vinavyohitajika na kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa wakati na hivyo muda wa mradi uliongezeka ambapo awali ulitarajiwa kukamilika mwaka 2018 na badala yake mradi ulikamilishwa mwaka 2023.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Wizara ya Maji Nishati na Maadini kwa kushirikiana na Shirika la Umeme kuendelea kusimamia taratibu zote zinazohitajika katika utekelezaji wa miradi ikiwemo taratibu za manunuzi ili miradi ifanyike kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa wakati na kuwanufaisha walengwa.

**Mradi wa Uimarishaji Maeneo Huru ya Uwekezaji**

Mradi wa Uimarishaji Maeneo huru ya Uwekezaji lengo lake ni kuendeleza maeneo maalumu yanayotambulika kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya 2023. Kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umemem na mawasiliano katika maeneo yote yaliyoainishwa ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Katika kuendelezwa maeneo Huru ya Uchumi inajumuisha uwekaji wa miundombinu muhimu ya Barabara, maji na umeme kwa Unguja na Pemba. Mradi huu ulianza mwaka 2021/2022 na unatarajia kukamilika 2025/2026. Mradi una maeneo Matano (5) ya utekelezaji ikiwemo Fumba, Mtaa wa Viwanda Amani, Bandari Huru, Maruhubi pamoja na Eneo Maalum la Uchumi Micheweni.

Eneo Maalumu la Uchumi Micheweni lilitangazwa kuwa ni eneo la uwekezaji mwaka 1992 ili kuchochea maendeleo ya Uchumi na kukuza huduma za kijamii. Eneo lina jumla ya hekta 808.8 na limegawika katika maeneo makuu mawili ambayo ni Block A (261.4 ha) na Block B (547.4 ha).

Kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 jumla ya fedha zilizotengwa ni TZS Bilioni 3.5 zilikusudiwa kutumika katika shughuli ya kujenga uzio na ofisi za Walinzi kwenye eneo la Block A Micheweni. Katika shughuli hizo zilizopangwa, kwa kipindi ambacho Kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji wake kwa upande wa Pemba, ilibaini kuwa kazi iliyokamilika ni ujenzi wa ukuta wa uzio uliojengwa na Kampuni ya Grasshopper Building Construction Ltd kwa jumla ya TZS 54,797,400/.

Kwa upande wa ujenzi wa Barabara 13.5 KM kwa kiwango cha lami. Katika ujenzi huo, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ilikubaliana na Kampuni ya IRIS Construction and Trade Limited ya Uturuki kuwa Mjenzi kwa gharama ya TZS 12,927,128,073.42 kwa muda wa miezi minne kuanzia tarehe 15 Agosti 2023 hadi tarehe 15, Disemba 2023. Hadi kufikia tarehe 15 Disemba, 2023 utekelezaji ulifikia asilimia 72 kutoakana na kuchelewa kuwasili kwa mtambo wa lami pamoja na hali ya mvua iliyojitokeza katika kipindi cha utekelezaji na kupelekea kutokukamilishwa kwa kazi hiyo kwa wakati.

## Changamoto Zilizobainika

i. Upatikanaji wa fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Barabara. Awali Wizara ilijpangia kutumia TZS Bilioni 6.9 kwa ujenzi wa Barabara yenye urefu wa 13.5 Km ambayo ilipangwa kukamilishwa na Wakala wa Barabara (ZANROAD). Kutokana na changamoto za kiutendaji zilizojitokeza na kupelekea kuvunja mkataba na ZANROAD, ZIPA iliingia mkataba na Kampuni binafsi ya IRIS kwa ukamilishaji wake.
ii. Ulipaji wa fidia ulikabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo kukosekana kwa

taarifa kamili kwa wanufaika wa fidia hizo kama kukosekana kwa vitambulisho, akaunti za benki na hivyo Wizara kuchukua jitihada za ziada za kuziomba taasisi za fedha kuwafungulia akaunti za muda mfupi kwa wasio na vigezo ili kukamilisha zoezi la ulipaji fidia.

iii. Uwepo wa makaazi na shughuli za kiuchumi katika maeneo maalum ya Uchumi ambapo katika ZONE A wananchi wanaendelea na shughuli za upandaji miti na katika ZONE B baadhi ya wananchi wamekuwa wakijenga na kuchimba matofali jambo ambali litaigharimu Serikali. Baadhi ya wananchi wamekuwa wakikaidi agizo la kutoendelea kuyatumia maeneo hayo licha ya Serikali kutoa tangazo rasmi la kutokufanyika kwa shughuli zozote za kudumu kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo maalum ya Uchumi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuendelea na juhudi ya kuielimisha jamii juu ya kuacha kufanya shughuli za kiuchumi na makaazi katika maeneo maalum ya uwekezaji na kufuata agizo la Serikali ya kutoendelea kuyatumia maeneo hayo ili Serikali itakapokuwa tayari kuyaendeleza maeneo hayo kutokupata gharama za kuwaondosha wananchi pamoja na kufanya malipo ya fidia wananchi hao.

ii. Kwa kuwa kumebainika changamoto ya kuvunjwa kwa mkataba baina ya ZIPA na ZANROAD katika ujenzi wa Barabara ya 13.5 km, Kamati inaitaka Wizara kuwa makini wakati wa kuingia mikataba ya utekelezaji wa shughuli za miradi pamoja na kuwa na usimamizi madhubuti utakaopelekea kufikia malengo ya kazi yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa kazi kwa muda uliopangwa na kwa kiwango kinachohitajika.

iii. Katika ujenzi wa Barabara kwenye maeneo huru ya Uwekezaji Micheweni, Kamati imeshauri kuwepo kwa majina katika Barabara hizo ili ziweze kuwaongoza watumiaji. Aidha, Kamati imeipongeza sana ZIPA kwa hatua ya ujenzi wa Barabara hizo ambazo imelifanya eneo hilo kuwa katika muonekano mzuri.

iv. Kamati imeshauri Barabara ya Micheweni Mjini kuingizwa katika Mpango kazi wa kuimarishwa Barabara hiyo mpaka kufikia eneo la mradi ili iendane na hadhi za Barabara zilizopo kwenye eneo la uwekezaji.

## Mradi wa Kuimarisha Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Park)

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kukuza, kusimamia na kuendeleza Sekta ya Biashara na Viwanda ili kuleta maendeleo nchini. Kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa matumizi ya TZS 28,417,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuimarisha maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks) na Mradi wa kuendeleza Uwanja wa Maonesho ya Kimataifa Zanzibar (Nyamanzi).

Mradi huu ulianza mwaka wa fedha wa 2019/2020 na kutarajiwa kukamilika kwake mwaka 2025/2026. Lengo la kuwepo kwa mradi huu ni kuvutia uwekezaji, kutengeneza ajira na kuongeza mauzo ya nje na kukabiliana na vikwazo vinavyozuia michakato ya ukuaji wa Viwanda Zanzibar.

Kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, kupitia mradi huu Wizara ilipanga kutumia TZS 26,012,000,000 kwa ajili ya kuendeleza maeneo tengefu ya viwanda ambayo ni eneo la Dunga na Pangatupu Unguja na eneo la Chamanangwe kwa upande wa Pemba.

Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Wizara ilipanga kutumia TZS 25,462,448,850 kwa kazi zake na hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imeingiziwa jumla ya TZS 5,662,887,268.27. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Barabara katika eneo la Viwanda kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 7.83 Gharama zilizotumika katika ujenzi huo ni TZS 23,367,869,925.58 pamoja na VAT na ulifikia asilimia 31 wakati Kamati ilipokuwa inapokea taarifa ya mradi huu.

Katika ujenzi wa miundo mbinu ya maji katika eneo la Dunga, Kamati ilielezwa kuwa kazi hiyo inafanywa na Kampuni ya Simba Developer Ltd na inajumuisha ujenzi wa mnara wa tanki la maji lenye uwezo wa lita milioni moja,uchimbaji wa visima na utandazaji wa bomba za maji kwenye eneo la Viwanda lenye ukubwa wa eka 173 kwa gharama ya TZS 3,467,975,475.75 pamoja na VAT.

### Changamoto Zilizobainika

i. Licha ya Jitihada za Serikali kuimarisha baadhi ya maeneo ikiwemo eneo la Chamanangwe Pemba kwa kuweka kwa baadhi ya miundombinu ambayo itawezesha kuanza kwa uzalishaji lakini Kamati ilipofanya ziara ilibaini kuwa uzalishaji katika eneo hilo bado haujaanza kufanyika jambo ambalo linarudisha

nyuma jitihada za Serikali za kuimarisha maeneo maalum ya viwanda kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza kipato cha mwananchi.

ii. Kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji wa mradi, imebaini kuwa kuna baadhi ya maeneo hayajapata wawekezaji. Miongoni mwa maeneo hayo ni Eneo la Dunga jambo ambalo Wizara inahitaji kulifuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa eneo hilo linapata muwekezaji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kushirikiana na Mamlaka ya kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) katika kutangaza maeneo tengefu ya Viwanda kwa kuwavutia wafanyabiashara wa nje na wa ndani katika kuyatambua maeneo hayo na kutumia fursa zilizopo kwa kufanya biashara ambazo zitasaidia katika kuchochea shughuli nyengine za Uchumi na ustawi wa wananchi wetu.

ii. Kamati inasisitiza Wizara juu ya kusimamia maeneo maalum ya viwanda kwa kuhakikisha kuwa, shughuli zilizopangwa kufanyika katika maeneo zinafanyika na zinaleta tija katika nchi yetu.

iii. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi katika maeneo ya Dunga na Chamanangwe pamoja na kuitaka Wizara kuhakikisha wanafuata mpango kazi huo katika utekelezaji wa shughuli zao kwa maeneo hayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho ya Kimataifa Zanzibar**

Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2020/2021 na kutarajiwa kukamilika mwaka 2023/2024. Lengo la mradi huu ni kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuweka eneo la kisasa kwa ajili ya maonesho ya kimataifa Zanzibar.

Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa kupitia mradi huu ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ikiwemo ujenzi wa ukuta, uwekaji wa miundombinu ya mashamiana makubwa na madogo, ujenzi wa vyoo pamoja na jengo la utawala.

Katika kufanikisha kazi hizo, Mkataba wa ujenzi baina ya Wizara na Jeshi la Kujenga Uchumi ni jumla ya TZS 5,462,599,464 pamoja na VAT na ambapo Kamati iliarifiwa kuwa, asilimia 70 ya fedha kwenye Mkataba tayari Wizara imelipa na hatua ya ujenzi

imefikia asilimia 80. Aidha, Kamati ilielezwa eneo lililobaki katika ujenzi ni jengo la utawala pamoja na kufanya maboresho katika eneo la ukumbi wa Mikutano.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kutokukamilika kwa baadhi ya kazi katika mradi ikiwemo kazi za ujenzi wa jengo la utawala pamnoja na kufanya marekebisho ya eneo la ukumbi wa mikutano.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuweka eneo la kisasa kwa ajili ya maonesho ya kimataifa Zanzibar jambo ambalo litasaidia katika kuitangaza Zanzibar pamoja na kuwapa fursa wafanyabiashara wa ndani kutangaza biashara zao na kupata masoko ya uhakika kupitia kituo hicho. Aidha, kwa upande mwengine Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili ukamilike utekelezaji wake kwa muda uliopangwa.

### Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Big Z)

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG – Z) ni programu ya miaka mitano iliyoanza utekelezaji wake tarehe 2 Disemba 2021. Gharama zilizopangwa ni jumla ya Dola za Kimarekani milioni 150 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu uliidhinishwa rasmi tarehe 10 Juni 2021 na kusainiwa tarehe 19 Agosti 2021 baina ya Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo kuu la Mradi huu ni kuimarisha hali ya Maisha ya Wananchi na kukuza maendeleo ya kiuchumi katika maeneo yaliyolengwa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 mradi wa BIG Z umepangiwa jumla ya TZS 22.8 bilioni. Kwa kipindi ambacho Kamati ilipata taarifa ya mradi huu, iliripotiwa kuwa, kwa kipindi cha miezi nane kuanzia Julai 2023 hadi Febuari 2024, jumla ya TZS 14.4 bilioni sawa na asilimia 63 ya fedha iliyopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 ziliingizwa katika mradi.

Mradi huu una sehemu nne ambazo ni Maendeleo ya Mjini na Miundombinu Jumuishi ambapo katika eneo hili linahusiana na uwekaji wa miundombinu na

huduma za msingi pamoja na mipango mbali mbali ya kuboresha maisha ya wakaazi wa maeneo ya Unguja na Pemba.

Kwa upande wa kujengea uwezo Taasisi za Serikali katika usimamizi na uendeshaji wa Miji na Kushajihisha Ubunifu katika eneo hili mradi unalenga katika kughramia kazi za kuimarisha uwezo wa taasisi za Serikali juu ya Utunzaji na usimamizi wa miji na kushajihisha matumizi ya Teknolojia na ubunifu katika kutekeleza majukumu yao.

Mradi pia una sehemu ya Uendeshaji, Ufuatiliaji na tathmini na kukabiliana na hali ya Dharura. Utekelezaji wa mradi huu unafanywa na taasisi tano (5) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Usimamizi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Taasisi zinazohusika moja kwa moja katika utekelezaji ni pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mita ana Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

### Changamoto Zilizobainika

i. Utekelezaji wa mradi huu unachukua muda mrefu kutokana na taratibu za manunuzi za Serikali na Benki ya Dunia ambapo taratibu hizo lazima zifuatwe ili kukamilisha utekelezaji wa mradi husika.
ii. Kunakuwepo na changamoto mbali mbali za maafa na za kimazingira ambazo zinajitokeza na kusababisha programu kuomba kufanya marekebisho yanayohitajika.
iii. Programu inahitaji utaalamu wa kimataifa ambapo mara nyengine hujitokeza kutokuendana na mazingira halisi ya Zanzibar.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango katika utekelezaji wa programu ya BIG Z kuwatumia vyema wataalamu wake wa ndani hasa katika masuala ya manunuzi pamoja na mikataba ili utekelezaji wa mradi uwe kwa ufanisi.

### Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) Kipindi cha Pili

Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ni Mpango wa Kitaifa ambao unatekelezwa kwa lengo la kuwaongezea kipato na fursa walengwa wa Mpango pamoja na kuboresha

mahitaji muhimu ya kimaisha ya kaya husika ikiwemo mahitaji ya chakula, malazi, mahitaji ya huduma ya elimu na afya kwa watoto wa kaya za walengwa.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbali mbali ambapo vipengele muhimu wanavyosimamia katika Mradi ni pamoja utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu katika maeneo yenye uhitaji mkubwa, utekelezaji wa uhaulishaji fedha kwa kaya za walengwa wa Mpango, utekelezaji wa Mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya pamoja na utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa.

### Changamoto Zilizobainika

i. Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Upenja kulijitokeza changamoto ya upatikanaji wa kifusi hali iliyopelekea kuchelewa kuendelea na utekelezaji wa mradi kwa muda uliopangwa.
ii. Kuchelewa kupatikana kwa mchango wa Serikali katika uendeshaji wa ofisi unaathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizopangwa.
iii. Kuwepo kwa baadhi ya wanufaika wa Miradi ya TASAF kwa upande wa Zanzibar kukosa fursa za kupata mkopo wa elimu ya juu kwa ajili ya kujiendeleza na masomo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuendelea kutoa elimu kwa Jamii katika namna ya kuibua miradi ya ujenzi katika maeneo yao ili iweze kuondoa changamoto wanazokabiliana nazo katika maeneo yanayotekelezwa miradi hiyo.
ii. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha utoaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi unafanyika kwa wakati ili kuepuka kucheleweshа utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa zinafanywa kwa wakati na kwa ufanisi.
iii. Kwa kuwa Kamati inaishauri TASAF Zanzibar na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHESLB) kufanya vikao kujadiliana kuhusu kuweka kipaumbele cha kuwapatia mikopo au ufadhili kwa ajili ya masomo ya juu wanafunzi ambao wanaotoka katika kaya maskini. Si jambo la busara kwa wanafunzi wanaotoka

katika kaya maskini kukosa mikopo ya elimu ya juu.

## Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Katika kufanikisha ujenzi wa Barabara na kuimarisha huduma za usafiri nchini, Serikali imepanga kujenga Barabara za Unguja na Pemba kupitia utekelezaji wa Programu ya Ujenzi wa Barabara kuu, Programu ya Ujenzi wa Barabara za ndani Pamoja na programu ya matengenezo ya Barabara za Mjini.

Utekelezaji wa Programu ya Ujenzi wa Barabara kuu unahusisha ujenzi wa Barabara nne. Barabara ya Tunguu – Makunduchi (48.5 km), Fumba – Kisauni (12km), Chake – Mkoani (43.5 km) na Barabara ya Chake – Wete (22.1 Km). Ujenzi wa Barabara hizi unajengwa na Kampuni ya Propav na Mecco Zanzibar Road Construction Limited kwa mkopo kutoka United Kingdom Export Finance kwa gharama ya Euro Milioni 230,798,792. Msimamizi wa ujenzi wa Barabara hizi ni Kampuni ya Dar al Handasah Consultants.

## Changamoto Zilizobainika

i. Wakandarasi walioingia mkataba wa Pamoja katika kazi ya ujenzi wa Barabara ya Tunguu – Makunduchi, Fumba – Kisauni na Chake -Mkoani ambao ni Kampuni ya Propav/Mecco walishitakiana Mahakamani na kutolewa hati ya Mahakama ya kusimamishwa kazi zote za mradi zisiendelee na hivyo mradi kushindwa kuanza kutekelezwa kwa muda uliopangwa.
ii. Kuongeza kwa gharama za ujenzi katika Barabara ya Chake - Wete kutokana na kuongezeka kwa kazi. Mwanzoni Barabara hii ilikusudiwa kufanyiwa matengenezo makubwa lakini wakati ujenzi ulipokuwa unaendelea, ilibainika kuwa ujenzi wake ufanyike kama ujenzi wa Barabara mpya. Hivyo, gharama ziliongezeka kutoka TZS 23,578.031,917 hadi kufikia TZS 26,618,162,917.
iii. Kubadilika kwa mchoro wa Barabara ya Chake – Wete kulipelekea kuongezeka kwa wananchi 16 ambao wanahitaji kulipwa fidia na hivyo Kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji ilielezwa kuwa, malipo ya fidia katika ujenzi wa Barabara bado hajakamilika ingawaje Wizara tayari imeshaomba malipo yao Serikalini.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara kuandaa mpango maalum wa kufuatilia wakandarasi

kupitia Kampuni wanazozifanyia kazi na mahusiano yao na wakandarasi wengine ili iwapo wakandarasi hao wataingia Mkataba wa pamoja (Joint Venture) katika kufanya kazi kunakuwa hakujitokezi changamoto ya kutofahamiana miongoni mwao na hatimae kukwamisha utekelezaji wa mradi kwa muda uliopangwa.

ii. Kamati inaitaka Serikali katika kuchagua Wakandarasi wa Ujenzi wa Barabara zake, kuwachagua kwa umakini mkubwa ikiwa ni Pamoja na kufahamu uzoefu wao katika kazi ikiwa ni pamoja na kupata kuona kazi zao za nyuma walizowahi kutekeleza ili hatimae kupata Wakandarasi wa uhakika ambao watakamilisha kazi kwa ufanisi na kwa muda uliokusudiwa.

### Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani

Ujenzi wa Barabara za ndani unahusisha ujenzi wa Barabara za vijijini zenye urefu wa kilomita 275.9 ambapo Unguja ni kilomita 140.95 na Pemba ni kilomita 134.95. Mradi ulianza tarehe 10 Machi 2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 10 Julai, 2025. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya AIRIS/ASER kutoka Uturuki. Gharama za mradi ni USD Milioni 80.3. Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS) ndio wasimamizi wa mradi huu. Programu hii ina lengo la kuunganisha mitaa na maeneo mbali mbali na Barabara kuu ili kupunguza msongamano katika Barabara kuu Pamoja na kupendezesha mji katika maeneo ya Zanzibar. Mradi huu unasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi zake zinatekeelzwa na kampuni ya AIRIS/ASER ya nchini Uturuki kwa gharama za TZS 44.060 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kupitia programu ya ujenzi wa Barabara za ndani, wakati wa utekelezaji wa Barabara ya Mfano (Mwera Police – Kibonde Mzungu) yenye urefu wa Km 6.1 ilibainika kuwa, ujenzi wake haukuwa wa kuridhisha na hivyo wakandarasi walitakiwa kufanya marekebisho wakati wakiendelea na ujenzi wa Barabara nyengine.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Wizara kuendelea na usimamizi wa karibu katika ujenzi wa Barabara unaoendelea ili kubaini kasoro za kiufundi zinazojitokeza na kusimamia

marekebisho yake ili utekelezaji wa mradi ukamilike kwa kiwango kinachotakiwa.

**Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini**

Programu ya Ujenzi wa Matengenezo ya Barabara za Mjini una urefu wa Kilomita 100.9. pia, unahusisha ujenzi wa Barabara za juu (Fly over) katika eneo la Amani na Mwanakwerekwe Round About, utanuzi wa Barabara kuu, ujenzi wa Barabara za ndani ya mji, ujenzi wa njia za watembea kwa miguu, taa za barabarani, taa za kuongozea magari (Trafic light), michoro ya kugawa Barabara (road marking), alama za barabarani za kuonyesha mipindo, kasi ya mwendo unaotakiwa na alama za wanaokatisha Barabara.

Ujenzi wa Barabara hizi unafanywa na Kampuni ya China Civil Engineering Construction Coorporation (CCECC) kutoka China na Msimamizi wa Ujenzi ni Kampuni ya Dar al handasah kutoka Lebanon. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 6 Agosti 2022 kwa gharama za fedha za Kimarekani USD 116,131,442.96 na kuanza rasmi tarehe 1 Disemba, 2022.

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Juni 2024, jumla ya kilomita 30.91 tayari zimewekwa lami na kilomita 15.9 tayari zimeshawekwa zege. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii ilipangiwa jumla ya TZS 80,100,000,000 kutoka Serikalini ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2024 fedha zilizotumika ni TZS 85,191,775,783.04 sawa na asilimia 106.3.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Serikali kulazimika kulipa fidia wananchi kutokana na kuwa, eneo la mradi linahusisha makazi ya wananchi na ambapo ili mradi uendelee kwa ufanisi, wananchi hao wanalazimika kuondoka katika maeneo hayo na kupisha utekelezaji wa mradi.
ii. Kamati imebaini kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya Wizara na Taasisi nyengine zinazohusika kwa namna moja ama nyengine katika utekelezaji unaoendelea wa ujenzi wa barabara hasa pale inapotokea uchelewaji wa kuondoa miundombinu ikiwemo ya nyaya za umeme, nyaya za simu au mabomba ya maji ili kuendeleza ujenzi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kwa kuwa Serikali imekuwa inapata gharama za kulipa fidia wananchi ili kupisha utekelezaji wa mradi, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuchukua juhudi ya kuhifadhi maeneo yake ikiwa ni Pamoja na kusimamia maeneo yake kwa mujibu wa mpango mji uliopangwa.
ii. Kamati inashauri Serikali kabla ya kuanza kutekelezwa miradi ya maendeleo, kuwepo na vikao vitakavyowashirikisha wadau wote wa eneo la mradi ili kuepusha kuwezesha mradi kutekelezwa bila ya mkwamo.

### Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya

Mradi wa ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi ulianza mwaka wa fedha wa 2023/2024 ambapo jumla ya TZS 20,000,000,000 zimetengwa. Hadi kufikia Juni 2024, jumla ya TZS 6,999,829,380 zimetumika sawa na asilimia 35.

Ujenzi huu wa Nyumba za Wafanyakazi ni kwa Unguja na Pemba ambapo Nyumba zitajengwa katika Hospitali ya Pangatupu, Kitogani, Mwera Pongwe, Vitongoji na Kinyasini. Lengo la ujenzi huo ni kuimarisha makaazi kwa Wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa utulivu, kuimarisha Utoaji wa huduma katika Hospitali hizo, kuongeza ufanisi na kusaidia uimarishaji wa mfumo wa rufaa kwa kuhakikisha kuwa, madaktari wanapatikana muda wote hata inapotokea dharura.

### Changamoto Zilizobainika

i. Nyumba zilizojengwa ni za vyumba viwili na kimoja hivyo kumebainika ufinyu wa nafasi katika Nyumba hizo ukilinganisha na mahitaji halisi ya familia ambayo ni makubwa kinyume na makisio yaliyofanywa.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza na kuiunga Mkono Serikali kwa dhamira yake njema ya kuwapatia makazi wafanyakazi madaktari. Kwa upande mwengine Kamati inaishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi kuzingatia mahitaji halisi ya walengwa kwani ujenzi wa Nyumba unaoendelea unakabiliwa na ufinyu wa nafasi hasa pale familia inapokuwa kubwa.

### Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya

Mahkama ya Zanzibar inatekeleza Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya kwa Unguja na Pemba. Jumla ya majengo saba (7) yanajengwa ambapo majengo manne (4) Unguja yanajengwa na Kampuni ya CRJE(East) Africa na kwa upande wa Pemba majengo matatu yanajengwa na Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

Gharama za Ujenzi kwa Unguja ni TZS 28,838,904,009.01. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 9,523,356,804.5 zinatumika kwa ujenzi wa jengo la Mahkama ya Mkoa wa Mjini Magharib (Mazizini) na jumla ya TZS 6,696,638,757.71 kwa ujenzi wa Tunguu Jengo la Mahkama wa mkoa wa kusini Unguja.

Pale Kiongele, jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja gharama za ujenzi ni TZS 6,696,638,757.71 na Kisakasaka Jengo la Mahkama Wilaya ya Magharib "B" Gharama za ujenzi ni TZS 5,922,269,689.
Katika utekelezaji halisi, Kamati imeelezwa kuwa ujenzi wa jengo la Mazizini umefikia asilimia 58, Jengo la Tunguu na Pale umefikia asilimia 70 na jengo la kisakasaka limefikia asilimia 54.

Kwa upande wa Pemba, ujenzi unahusisha majengo matatu (3) na unatekelezwa na Mkandarasi wa kikosi cha JKU. Jumla ya gharama zinazotarajiwa kutumika ni TZS 14,001,736,292.11. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 3, 664,298,094.18 zinatumika kwa Changaweni Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kusini Pemba, kiasi cha TZS 6,673,140,103.75 ni gharama kwa ujenzi wa Kinyasini Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba na TZS 3,664,298,094.18 ni gharama za ujenzi wa Konde Jengo la Mahkama ya Wilaya ya Micheweni Pemba.

Katika utekelezaji uliofanyika, ujenzi wa Mahkama ya Wilaya ya Mkoani umefikia asilimia 40, ujenzi wa mahkama ya Wilaya ya Konde umefikia asilimia 67 na ujenzi wa jengo la Mahkama ya Mkoa liliopo Kinyasini umefikia asilimia 72.8.

### Changamoto Zilizobainika

i. Utekelezaji wa mradi ulikabiliwa na msimu wa mvua kubwa katika kipindi cha Disemba mpaka Febuari na kupelekea kutokufanyika kwa baadhi ya kazi.
ii. Kujitokeza kwa tatizo la umeme kwa nyakati tofauti ambapo Mkandarasi wa Unguja CRJE amekuwa akiripoti tatizo la umeme katika eneo la Tunguu na Mazizini na kupelekea machine kutokufanyika kazi ipasavyo.

iii. Suala la upatikanaji wa mchanga kwa ajili ya kazi ulikuwa si nzuri na kupelekea kuchelewa kwa kazi mpaka pale ambapo mchanga wenye sifa na ubora unapopatikana.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Mahkama kupangilia ratiba zake za utekelezaji wa kazi za mradi kwa umakini ili kufidia vipindi vya mvua kubwa ambapo muda huo, kazi huwa hazifanyiki ipasavyo.
ii. Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuzipa mashirikiano ya karibu taasisi zake zinazotekeleza miradi hasa pale zinapokuwa zinakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa mali ghafi. Aidha, suala la upatikanaji wa umeme kwa viwango vinavyotakiwa, Kamati inasisitiza sana jambo hili ili kurahisisha utekelezaji wa miradi mbali mbali nchini.

### Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kukuza na kuendeleza sekta ya Viwanda kwa lengo la kuleta Maendeleo nchini. Katika utekelezaji wa majukumu yake wizara inatekeleza mradi wa kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda ambao lengo lake ni kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda ili kuvutia uwekezaji, kuzalisha ajira, kuongeza mauzo ya nje ya nchi na kurahisisha uwekaji wa Viwanda Zanzibar.

Kwa mwaka wa 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa matumizi ya TZS 26,012,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Miongoni mwa kazi zilizofanywa kupitia mradi huu ni pamoja na uandaaji wa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi kwa eneo la Viwanda la Dunga Zuze Unguja na Chamanangwe Pemba, usimamizi wa ujenzi wa barabara na mradi wa Miundombinu ya maji na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika eneo la Dunga Zuze.

Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 Wizara imeidhinishiwa jumla ya TZS 40,320,000,000 kwa ajili ya kuyaendeleza maeneo ya Dunga, Chamanangwe na Pangatupu. Katika kutekeleza Kazi kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Kamati iliarifiwa kuwa, wizara inaendelea na taratibu za zabuni ya kumtafuta Mshauri Elekezi wa kuandaa michoro ya ujenzi wa barabara, miundombinu ya maji, ukuta na majengo

ya Viwanda.

## Changamoto Zilizobainika

i. Wizara kushindwa kutekeleza kazi za uandaaji wa Mpango wa Utunzaji mazingira na jamii kwa eneo la Pangatupu, ujenzi wa ukuta na Majengo ya Viwanda kutokana na kukosekana kwa hati miliki ya eneo la Pangatupu.
ii. Uhaba wa bajeti umechangia kutokufanyika kwa kazi za ujenzi wa ukuta na majengo ya Viwanda.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Wizara kuendelea na taratibu za kufuatilia upatikanaji wa hatimiliki katika eneo la Pangatupu ili utekelezaji wa mradi uweze kufanyika kama ulivyopangwa na uweze kuleta manufaa kwa jamii.

## Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Maonesho Dimani Fumba

Wizara ya Biashara Maendeleo ya Viwanda inatekeleza mradi wa kituo cha Maonesho Dimani ili kuimarisha mazingira bora ya ufanyaji Biashara na kuimarisha uchumi nchini, kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati kutumia eneo hilo kutangaza bidhaa na huduma wanazotoa. Kwa mwaka wa fedha wa 2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 10.00 bilioni kutoka fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa upande wa utekelezaji, Wizara iliingia makubaliano na Mkandarasi mzawa (Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar) kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya msingi ikiwemo ujenzi wa ukuta katika eneo la Kituo cha Maonesho, vibaraza vya kuwekea mashamiana makubwa na madogo na eneo la kuhifadhia vifaa vya maonesho, ujenzi wa vyoo pamoja na ujenzi wa jengo la utawala. Utekelezaji halisi wa kazi umefikia asilimia 80 ambapo baadhi ya kazi bado hazijakamilika ikiwemo ujenzi wa jengo la utawala ambao umefikia katika hatua ya msingi (foundation).

## Changamoto Zilizobainika

i. Kuongezeka kwa gharama za ujenzi zilizowasilishwa na Mkandarasi na kufikia TZS 13.001 bilioni badala ya bei ya awali ya TZS 5.462 bilioni waliyokubaliana na Wizara. Hivyo, imepelekea kutoendelea kwa ujenzi kutokana na kutokuwafikiana

baina ya Mkandarasi na Wizara.

ii. Kukosekana kwa fedha za maendeleo kumechangia baadhi ya kazi kutoweza kukamilishwa. Miongoni mwa kazi ambazo hazijakamilishwa ni pamoja na ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia vifaa na kuimarisha mfumo wa maji machafu na kujengea eneo la kuhifadhia taka.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuanzisha Kituo cha Biashara ili kutoa fursa ya kujitangaza kwa wafanya Biashara wa aina mbali mbali. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuwasimamia kwa karibu wafanyabiashara hao ili waendane na dhamira ya kufunguliwa kwa kituo hicho pamoja na kuendelea kuwasimamia katika ufanyaji wa Biashara zao.
ii. Kwa kuwa kumejitokeza changamoto ya kutokukubaliana kwa Mkandarasi na Wizara, Kamati inaiomba Serikali kulitafutia ufumbuzi suala hili ili utekelezaji wa mradi uweze kufanyika kwa muda uliopangwa pamoja na kuwapa tija wananchi.

**Programu ya Uimarishaji wa Ubora wa Elimu**

Programu ya Uimarishaji wa Ubora wa Elimu ni miongoni mwa programu zinazotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuimarisha utekelezaji wa mipango ya sekta ya elimu kwa ufanisi nchini. Programu ilianzishwa ili kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote kwa kuwapatia walimu na wanafunzi vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na mafunzo ya walimu na matumizi ya TEHAMA.

Fedha za utekelezaji wa programu ya uimarishaji wa elimu zinatokana na mchango wa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya TZS 25.29 bilioni zilipangwa kutumika katika kipindi cha Julai – Disemba kwa mwaka wa 2024/2025. Kati ya hizo TZS 17.15 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.14 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Disemba, 2024, Kamati iliarifiwa kuwa utekelezaji wa programu ulitumia jumla ya TZS 6.11 bilioni sawa na asilimia 24.2.

Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia programu hii ni pamoja na:

i. Kuzipatia skuli za Sekondari vifaa kwa ajili ya masomo ya fani ya ujuzi wa amali na ufundi.
ii. Kuzipatia skuli vifaa vya TEHAMA vikiwemo komputa za mezani 500, laptop 100

na smart board 20. Vifaa hivyo vinatarajia kugharimu kiasi cha USD 1,073,215.54 kwa mujibu wa mkataba.

iii. Kuzipatia Skuli vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum

iv. Kuwaandaa walimu wa mafunzo ya fani za amali na ufundi kwa kuwapatia mafunzo. Miongoni mwa walimu ambao watapatiwa mafunzo ni pamoja na walimu wa skuli za ufundi za Mikunguni na Kengeja. Aidha, mafunzo ya walimu katika utekelezaji wa mtaala mpya wa Sekondari yatakayohusisha masomo ya jumla (general subjects) na mkondo wa mafunzo ya amali na ufundi

v. Kuziunganisha Skuli 230 za Sekondari na Mkonga wa Taifa ambapo katika utekelezaji wake, Wizara imeanza matayarisho ya zoezi la kuziunganisha Skuli na Mkonga wa Taifa kama ni sehemu ya Mkakati wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika elimu.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati kwenye baadhi ya miradi na kupelekea kushindwa kutekelezwa kwa wakati kwa ufanisi. Fedha zilizopatikana kwa kipindi ambacho Kamati ilifuatilia utekelezaji wake zilifikia asilimia 24.2 ambayo ni fedha ndogo katika kukamilisha malengo yaliyokusudiwa.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha kwenye programu ya uimarishaji wa elimu, Kamati inaitaka Wizara kuendelea na jitihada ya kusimamia programu hii kwa kuomba fedha Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wake kwa muda uliopangwa pamoja na kufikia malengo.

### Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (OMKR)

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeendelea kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa miradi mbalimbali katika sekta ya mazingira ambayo inafadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Miradi inayotekelezwa na Ofisi hii ni pamoja na:

i. Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira

ii. Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani, na
iii. Mpango wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani.

**Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira**

Mradi huu umeanza rasmi mwezi wa Disemba 2024 na unategemewa kukamilika mnamo mwezi wa Mei 2025 chini ya Usimamizi wa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA). Lengo kuu la Mradi ni kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuzuia maji ya Bahari kuingia katika eneo linalotumika kwa shughuli za kilimo ambalo linatumiwa na familia 60 zenye idadi ya watu wanaofikia 360 na wanaojishughulisha zaidi na ukulima wa mazao ya mihogo na migomba.

Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 mradi umepangiwa jumla ya TZS 500,000,000/= kupitia fedha za SMZ ambapo jumla ya TZS 298,508,950/= zimepatikana. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 118,150,500/= sawa na asilimia 53% zimetumika kumlipa Mkandarasi wa Kampuni ya Kin Investment. Wakati Kamati ilipopokea taarifa za Utekelezaji wa mradi huu, iliarifiwa kuwa, hatua za awali za ujenzi zimeshaanza ambapo ujenzi umefikia asilimia 53%.

**Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani**

Mradi huu utekelezaji wake ni wa muda wa miaka mitatu kuanzia 2022/2023 hadi 2024/2025. Unatekelezwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo pamoja na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Fedha za utekelezaji wa Mradi ni TZS 2.4 bilioni. Lengo la Mradi ni kujenga uwezo wa wakulima wadogo wadogo kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakuwa na matokeo yenye tija. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika kupitia mradi huu ni pamoja na:

i. Ujenzi wa tuta la kuzuia maji ya cumvi kuingia kwenye bonde la Kilimo cha Mpunga la Tovuni, lenye urefu wa mita 400
ii. Ujenzi wa msingi wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 950 katika bonde la Tovuni
iii. Mafunzo ya Ufugaji nyuki, upandaji na uhifadhi wa mikoko na miti ya misitu kwa

wanajamii wa eneo la mradi. Jumla ya washiriki 119 wamepata mafunzo.

**Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizra ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wanatekeleza mradi huu wa miaka 10 ambao utekelezaji wake utakuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2023/2024 hadi 2033/2034.

Lengo kuu la Mradi ni kuhamasisha na kuwawezesha wananchi wote wa Zanzibar na wadau kuelewa umuhimu wa misitu, uhifadhi wa miti iliyopo, kuipanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae sambamba na uhamasishaji wa matumizi ya nishati mbadala kwa jamii ili kupunguza gesi joto ambalo linaleta athari katika mabadiliko ya tabia nchi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Katika utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani, fedha za utekelezaji wa mradi huu zinatoka kwa washirika wa maendeleo lakini kumejitokeza changamoto ya upatikanaji wa fedha hizo. Licha ya TZS 547,083,840 kupangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2024, hadi Kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji wa mradi huu, hakukuwa na fedha yeyote iliyopatikana.
ii. Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji na ukaguzi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani, Kamati inashauri watendaji wanaosimamia mradi huu kufuatilia kwa karibu na kufahamu sababu zinazopelekea kutokupatikana kwa fedha hizo na hatimae waweze kujipanga namna ya kukabiliana nazo na kuweza kuendelea na utekelezaji wa mradi kwa muda uliopangwa.
ii. Kwa kuwa suala la ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ni jambo la lazima katika kufanikisha utekelezaji wa mradi kwa kiwango kinachotakiwa, Kamati inaitaka Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kuendelea kufuatilia utaratibu wa upatikanaji wa vyombo vya usafiri katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili

kuondoa changamoto ya vyombo vya usafiri na kuweza kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi yao.

### Miradi ya Iliyotekelezwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU)

Wizara ya uchumi wa Buluu katika kutekeleza majukumu yake inahusisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo inakwenda sambamba katika kufikia lengo kuu la Wizara la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu la kusimamia na kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari na kuwawezesha wajasiriamali kwa mbinu tofauti ikiwemo ya kuwapatia elimu.

Miongoni mwa miradi ambayo Kamati ilifuatilia utekelezaji wake ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Samaki ya Kisasa, Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini na Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini kwa kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025.

### Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki

Lengo la Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki ni kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea miundombinu ya kuhifadhia na kuuzia Samaki yenye hadhi ya kisasa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Mradi unatekelezwa eneo la Fungurefu kwa Unguja na Mkoani kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa Fedha wa 2024/2025 mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 27,000,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 14,684,100,000 kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Hadi kufikia Disemba 2024, jumla ya TZS 3,101,511,260 zimepatikana na kutumika sawa na asilimia 21 ya makadirio. Miongoni mwa utekelezaji uliofanyika kwa Mkoani ni pamoja na kukamilisha kumtafuta Mshauri Elekezi na Mkandarasi pamoja na michoro na kuendelea na hatua za ujenzi wa Jengo la Biashara na Ofisi. Aidha, ujenzi wa maeneo ya maduka na vyoo vya watumiaji uaendelea.

Kwa upande wa Unguja, katika ujenzi wa Diko na soko la Samaki Fungurefu,

matayarisho ya ujenzi yamaekamilika na Mkandarasi ameshapatikana na kukabidhiwa eneo kwa ajili ya ujenzi.

### Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini

Mradi una lengo la kuborsha miundombinu ya maabara ya uthamini wa ubora wa bidhaa baharini. Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4,000,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2024 mradi umeingiziwa na kutumia jumla ya TZS 728,472,242 sawa na asilimia 18 ya makadirio ya fedha zilizotumika katika kufanya malipo ya awali kwa wazabuni kama ilivyo katika makubaliano ya mkataba kwa ajili ya kusambaza mashine kubwa za maabara pamoja na vifaa vya maabara ya Microbailojia. Kwa upande wa ujenzi wa uzio katika jengo la maabara ya uthamini, Taasisi imefanikiwa kumpata mjenzi wa ukuta, kibanda cha Mlinzi na tanuri la kuchomea taka sumu ambapo eneo la ujenzi limeshakabidhiwa kwa Mkandarasi na utekelezaji uanendelea.

### Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Mradi jumuishi wa uwezeshaji wa wanawake katika ufugaji wa mazao ya baharini una lengo la kuwawezesha wakulima wa mwani na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu ya mnyororo wa thamani. Mradi umeanza mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/2027. Mradi unatarajiwa kutumia gharama za Dola za Kimarekani Milioni 5.5 hadi kukamilika kwake, fedha za Mradi ni kutoka kwa Shirika la Maendeleo KOICA. Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2,400,000,000.

Miongoni mwa kazi zilizopangwa kupitia mradi huu ni pamoja na kuanzisha mashamba manne ya majaribio ya mwani, ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani Chokocho Pemba, kutoa mafunzom kwa wanawake 2,000 wakulima wa mwani na majongoo Bahari.  Kwa upande wa fedha, kwa kipindi cha Julai _ Disemba ambacho Kamati kilifuatilia utekelezaji wake hakukuwa na fedha iliyopatikana.

### Changamoto Zilizobainika

i. Upatikanaji mdogo wa fedha za Miradi ambapo katika Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki fedha iliyopatikana ni asilimia 21 ya

makadirio, Mradi jumuishi wa uwezeshaji wa wanawake katika ufugaji wa mazao ya baharini fedha iliyopatikana ni asilimia 18 ya makadirio na Mradi jumuishi wa uwezeshaji wa wanawake katika ufugaji wa mazao ya baharini hakukuwa na fedha iliyopatikana wakati Kamati ilipofanya ufuatiliaji. Hali hii inapelekea kutokufanyika kwa kazi zilizokusudiwa za Mradi.

ii. Uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi kama vile gari na pikipiki kwa Idara na Taasisi za Wizara unarudisha nyuma utekelezaji wa kazi hasa za ufuatiliaji wa miradi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha za miradi kwa wakati ili kuzuia ucheleweshaji wa utekelezaji na kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Hii inaweza kufanikishwa kwa kuimarisha mipango ya bajeti, kuongeza vyanzo vya mapato, kuhakikisha miradi inawekewa kipaumbele kulingana na umuhimu wake na kutekelezwa kwa awamu na sio miradi kwa wakati mmoja, na kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo ili kupata vyanzo mbadala vya fedha. Pia, ni muhimu kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha fedha zinapatikana na kutumika ipasavyo kwa maendeleo ya sekta husika.

ii. Uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi kama vile vyombo vya usafiri unaathiri sana utekelezaji wa kazi, hasa ufuatiliaji wa miradi. Hali hii inapelekea wasimamizi wa miradi kushindwa kufika maeneo ya miradi kwa wakati na kufanya ukaguzi unaohitajika. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inapaswa kufanya tathmini ya mahitaji ya miradi kuanzia hatua za awali, usimamizi wake na namna utekelezaji utakavyofanyika mpaka kukamilika kwa mradi, kuandaa mpango wa ununuzi, kutenga bajeti maalum, kuimarisha usimamizi wa matumizi, na kutafuta vyanzo mbadala. Kwa kuchukua hatua hizi, Serikali itakuwa na uhakika miradi ya maendeleo itaweza kutekelezwa kwa ufanisi.

### Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Programu ya kuendeleza viwanja vya michezo ni programu ya Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya programu ndogo ya ukuzaji na uendelezaji wa michezo Zanzibar. Lengo la Programu hii ni kuiwezesha sekta ya michezo kujenga na kuimarisha

muindombinu ya michezo Zanzibar inayokidhi viwango vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Programu hii imeanza katika mwaka wa fedha 2021/2022 na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ilipangiwa jumla ya TZS bilioni 51.25 kati ya fedha hizo, TZS 49.97 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.28 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko la bajeti ya ziada katika utekelezaji wa Mradi.

ii. Baadhi ya maeneo ya ujenzi wa viwanja kuwa madogo kwa mujibu wa mahitaji ambapo hupelekea kubadilisha maeneo na pia kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kwa wakati.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Licha ya Serikali kuleta maendeleo katika sekta ya michezo nchini, lakini pia kuna taratibu zinahitajika kufuatwa ili kurahisisha utekelezaji wa miradi inayoendelea katika sekta hiyo. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kufuata taratibu zilizowekwa wakati wa kuhitajika Bajeti ya ziada ili kuondosha utata utakaojitokeza wakati wa ufuatiliaji wa utekelazaji wa Bajeti katika Wizara husika.

ii. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kunafanyika uhakiki wa maeneo yatakayotumika kwa ajili ya ujenzi pamoja na kuzingatia baadhi ya mahitaji katika hatua za awali kabla kuanza kwa mradi ili kuepusha ongezeko la fedha za ziada.

### Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu, Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani na Programu ya Matengeneo ya Barabara za Mjini

Sekta ya barabara ni moja ya nguzo kuu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yeyote. Barabara kama njia kuu ya usafiri, zina mchango mkubwa katika kuuunganisha maneneo tofauti, kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na huduma pamoja na kuboresha ya watu kwa ujumla. Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi katika kuhakikisha inaimarisha huduma za usafiri wa barabara Unguja na Pemba, imepanga kuzijenga barabara mbali mbali pamoja na kuzifanyia

matengenezo barabara za Mjini. Ili kufanikisha ujenzi wa barabara hizo, Wizara imezigawa katika Programu mbali mbali ikiwemo Programu ya Ujenzi wa barabara za ndani, Programu ya ujenzi wa barabara Kuu pamoja na Programu ya matengezo ya barabara za mjini.

**Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu Utekelezaji wa Barabara za Tunguu – Makunduchi, Fumba Kisauni na Chake Chake – Mkoani**

Programu hii inajumuisha ujenziwa barabara Kuu (4), Barabara ya Tunguu – Makunduchi (53 km), Barabara ya Fumba – Kisauni (12 km), Barabara ya Chake – Mkoani (43.5 km) na Barabara ya Chake – Wete (22.1km) ambapo utatamia jumla ya Euro Milioni 230,798,792. Hatua za Utekelezaji wa barabara hizi za Tunguu – Makunduchi, Fumba Kisauni na Chake Chake Mkoani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umekumbana na changamoto ambayo imepelekea kuvunjika kwa mkataba wa pamoja ambao ulikuwa baina ya Kampuni ya MECCO na Kampuni ya PROPAV hali iliyopelekea kutokuendelea kwa kazi ya ujenzi. Hatua iliyochukuliwa ni kugawana maeneo ya kazi kila kampuni na sehemu yake ya kufanyia kazi.

**Programu ya Ujenzi Barabara ya Chake – Wete 22.1km**

Utekelezaji wa barabara hii unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 26,618,162,917 ambapo utajengwa kwa urefu wa kilomita 22.1 na upana wa mita 6. Ujenzi wa Barabara hii ulilazimika kufanyiwa matengenezo makubwa kutokana na asili yake hali iliyopelekea ni sawa na kuijenga upya kwani baadhi ya maeneo ya barabara hii kwa kuanzia Ziwani hadi Bahanasa ililazimika kubadilishwa mchoro wa awali ili kukwepa kuondolewa kwa umeme mkubwa ambao unapatika katika maeneo hayo hali iliyopelekea kuongezeka kwa muda wa utekelezaji wa ujenzi huo na kupelekea kukamilika mwezi Januari 2025. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni 2024 jumla ya kilomita 14.5 tayari zimewekwa lami kuanzia Meli tano hadi Mzambarauni.

**Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani**

Programu hii inahusisha ujenzi wa Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya miji na vijiji ambapo Unguja ni kilomita140.95 na kwa upande wa Pemba ni kilomita 134.95. Programu hii ina lengo la kuunganisha mitaa na maeneo mbali mbali na barabara kuu ili kuweza kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kupendezesha miji katika maeneo ya Zanzibar. Mradi huu

unasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi zinatekelezwa na Kampuni ya AIRIS/ASER ya Nchini Uturuki kwa gharama za TZS 44,060,000,000/ kutoka Serikalini.

### Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

Katika Programu hii, Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Kampuni ya China Civil Engineering Construction Company CCECC pamoja na Msimaizi wa ujenzi kampuni ya Dar – al – handasah kutoka nchini Lebanon kwa pamoja wameamua kuzifanya matengenezo barabara hizi ambapo mradi huu utahusisha ujenzi na utanuzi wa barabara Kuu, ujenzi wa barabara za ndani ya Mji, ujenzi wa njia za watembea kwa miguuzenye urefu wa kilomita 100.9 Pamoj na ujenzi wa barabara za juu Fly over katika maeneo ya Mwanakwerekwe na eneo la Amani lengo ni kurahisisha usafiri pamoja na kutatua changamoto ambazo zinawakabili wananchi katika njia hii ya usafiri. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Juni 2024, jumla ya kilomita 30.91 tayari zimewekwa lami na kilomita 15.9 tayari zimeshawekwa zege. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii ilipangiwa jumla ya TZS 80,100,000,000 kutoka Serikalini ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2024 fedha zilizotumika ni TZS 85,191,775,783.04 sawa na asilimia 106.3.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya Wizara na Taasisi nyengine zinazohusika kwa namna moja ama nyengine katika utekelezaji unaoendelea wa ujenzi wa barabara hasa pale inapotokea uchelewaji wa kuondoa miundombinu ikiwemo ya nyaya za umeme, nyaya za simu au mabomba ya maji ili kuendeleza ujenzi.

ii. Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko kwa wananchi waliopisha ujenzi wa barabara kutokukamilishiwa malipo yao ya fidia.

iii. Suala zima la uzingatiaji wa mitaro ambayo itasaidia suala zima la kutuwama kwa maji katika badhi ya maeneo ambayo ujenzi wa barabara unaendelea nalo ni changamoto ambayo imekuwa ikizungumziwa sana na wananchi wa baadhi ya maeneo.

iv. Uchelewaji wa uwekaji wa alama za barabarani katika barabara ambazo tayari zimekamilika pia limekuwa likitiliwa mkazo na wananchi ili kukwepa ajali ambazo zinaweka kuepukika hususan katia njia za ndani ambapo wananchi wamekuwa wakipita kwa kasi sana.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaita Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kuwa na mashirikiano ya karibu katika kutatua suala zima la uwondoaji wa nyaya zozote ambazo zitaathiri utekelezaji mzima wa ujenzi wa barabara.

ii. Kamati inawataka wananchi kutunza barabara zote zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa kuweza ili kuweza kudumu kwa muda mrefu kwa maslahi ya kizazi cha sasa na cha baadae.

iii. Kamati inaitaka Wizara kuzingatia umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kwa kuweka mitaro pembezoni mwa barabara ili kuondokana na kutuwama kwa maji na kuweza kudumu kwa muda mrefu pamoja na kuleta haiba nzuri ya mijini na vijijini.

iv. Kwa kuzingatia usalama wa barabarani na kukwepa ajali zisizo za lazima, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha uwekaji wa alama za barabarani ili kunusuru ajali ambazo zinaweza kuepukika.

**Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutekeleza Programu ya Umwagiliaji Maji ambayo inahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo misingi ya saruji yenye urefu wa kikomita 43.7, misingi ya kutolea maji ya ziada pamoja na ofisi moja kwa kila bonde ukubwa wa hekta 1053 (Eka 2,632.5) katika mabonde ya Cheju A, Mlemele, Kinyasini, Kilombero,Chaani na Kibokwa. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS bilioni 33.584 ambazo zinahusisha ulipaji wa mishahara kwa jumla ya TZS 1.470 bilioni, ulipaji wa matumizi mengineyo jumla ya TZS milioni 412.800 na TZS 31.701 bilioni kwa ajili ya maendeleo ambazo TZS bilioni 31.701 kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS milioni 500 ni mchango kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Juni 2024 Programu hii ilipata jumlaya TZS 22.833 bilioni sawa na asilimia 67 ya fedha zilizoidhinishiwa na hakukuwa na mchango wowote kutoka Serikalini.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ilipangiwa jumla ya TZS TZS bilioni 27.698 ambapo TZS bilioni 2.198 ilihusisha ulipaji wa mishahara, matumizi mengineyo na fedha za maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo ambazo ni TZS bilioni 25.500. Hadi kufikia mwezi Disemba 2024 Programu imeingiziwa jumla ya TZS bilioni 32.738 sawa na asilimia 121.62.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kamati imebaini kuwa mbali na juhudi zilizochukuliwa na Wizara kuandaa mradi huu wa umwagiliaji ambao utawawezesha wananchi kuendeleza kilimo chenye tija lakini pia wananchi hao wanakabiliwa na uchache wa mbolea hali inayowapelekea kununua mbolea kwa kuchangishana kupitia kamati za Mabonde.

ii. Kamati imebaini uhaba wa fedha za maendeleo kutoka Serikalini zimecheleweshа shughuli zilizopangwa katika utekelezaji wa Mradi wa umwagiliaji hasa uungaji wa umeme mkubwa pamoja na malipo ya fidia.

iii. Ufikaji wa maji katika mabonde umekuwa wa kusuasua kutokana na mfumo uliopo ambao huchukua muda mrefu kuwafikia wakulima wengine.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa Miradi ambayo inatekelezwa kuhusiana na kilimo kuzingati pia upatikanji wa mbolea za kutosha ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao

ii. Kufuatilia uhaba wa fedha za miradi kutoka Serikalini, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo unakwenda sambamba na shughuli zote zilizopangwa ili kurahisisha utekelezaji.

iii. Suala jengine ambalo Kamati inaendelea kutoa msisitizo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji katika jengo la scheme liliopo katika bonde la Mlemele.

iv. Kamati inatoa wito kwa wananchi wote ambao wamenufaika na Mradi huu wa

umwagiliaji waji kuhakikisha wanaitunza misingi iliyojengwa kwa kuifanyia usafi ili kuweza kurahisisha maji kufika katika maeneo husika.

**Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Masheha Unguja na Pemba**

Kufuatia changamoto zinazowakabili masheha katik kuwahudumia wananchi katika ngazi ya Shehia pamoja na kuweka kumbukumbu za kiofisi zinazohusiana na Taarifa zinazohusiana na wananchi, Masheha walilazimika kutumia nyumba zao kama Ofisi hali ambayo inapelekea kutokupatikana kwa usiri wa Taarifa hizo. Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeamua kuanzia ujenzi wa nyumba za Masheha ili kuweza kupata faragha ya shughuli zao za kila siku.

Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza iljumuisha ujenzi wa Ofisi 64 kwa Unguja na Pemba. Katika kipindi hichi Mradi uligharimu jumla ya TZS 3,120,419,200 kutoka Serikalini.

Katika awamu ya pili, Mradi uligharimu jumla ya TZS 2,292,732,000 kutoka Serikalini ambazo zitatumika katika kujenga Ofisi 48 kati ya hizi, 20 zitajengwa katika Shehia za Pemba na Ofisi 28 zitajengwa katika Shehia a Unguja. Katika ujenzi huu unajumuisha pia ununuzi wa samani za ndani.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Mbali na juhudi zilizochukuliwa na Serikali za kuhakikisha masheha wa Shehia husika wanapatiwa Ofisi za kutekeleza majukumu yao lakini bado Wizara inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maeneo ambayo yatakwenda kuanza ujenzi wa Ofisi hizo hususan maeneo ya Wilaya ya Mjini.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kwa kuzingatia umuhimu wa utunzaji kumbukumbu na usiri wa Taarifa za wananchi, Kamati inashauri Wizara kuja na Mpango Mkuu utakaowezesha upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa Ofisi za Masheha ili kuwawezesha kutekelza majukumu yao kwa ufanisi na mkubwa.

ii. Kuhusiana ujenzi wa Ofisi hizo, Kamati inashauri uwende sambamba na mifumo iliyopo kwa sasa ili kuwawezesha Wizara husika kupata taarifa moja kwa moja zinazohusiana na wananchi wa Shehia husika.

## Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM na Mradi wa Uzamiaji na Uwokozi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Kilianzishwa chini ya sheria nambari 1 ya mwaka 2003 ambacho kina jukumu la kulinda na kuhakikisha ulinzi na usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kufanya kazi za uwokozi baharini, kuzuia makosa yote yanayofanyika upande wa baharini, kulinda rasilimali za bahari, kusafirisha na kulinda misafara ya viongozi baharini pamoja na kushirikiana na jeshi la wananchi pale inapohitajika hivyo katika kuilinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kutekeleza Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM, kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Kikosi kiliidhinishiwa jumla ya TZS 2,650,000,000 ambao zimetumika katika kukarabati, ununuzi wa samani pamoja na usambazaji wa vifaa katika Hospitali ya KMKM iliyopo Gando.

Utekelezaji wa Mradi wa Uzamiaji na Uwokozi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kikosi kiliidhinishiwa jumla ya TZS 2,460,040,000 ambazo zitatumika katika kupelekea chelezoni vyombo vyote vikubwa viwili, hadi Kamati inapokea Taarifa hii, Mradi wa Uzamiaji na Uwokozi upo katika hatua ya kusubiri kusainiwa kwa mkataba na mradi kuana kutekelezwa.

### Changamoto Zilizobainika

i. Uchelewaji wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa Miradi umekuwa ni changamoto kubwa kwa upande wa KMKM hali inayopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kwa wakati.

ii. Kuchelewa kwa hatua za awali za utekelezaji wa Mradi kwa upande wa KMKM nako pia kunacheleweshа kuanza kwa utekelezaji wa Mradi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Ili kuimarisha mazingira bora kwa Wapiganaji wetu wa KMKM, Kamati inashauri uzingatiaji wa utoaji wa fedha za miradi kwa wakati ili kuwezesha utekeelzaji wa miradi hiyo.

ii. Kamati inashauri kufuata taratibu zote za awali ambazo ndio msingi wa kuanza kwa Miradi ili kurahisisha pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji.

**Mradi wa Kijani Pemba (Green & Smart Cities "SASA")**

Mradi wa Green & Smart Cities unafadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya EU, Mradi huu unatekelezwa na Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGO) kwa mashirikiano ya pamoja na Taasisi za Serikali ambazo kwa Mradi huu ni Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Afisi ya Rais – Fedha na Mipango. Utekelezaji wa mradi huu kwa upande wa Pemba unatekelezwa katika maeneo ya Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni. Utekelezaji wa Mradi huu utagharimu jumla ya EURO 5,533,019.91 sawa na Shilingi 11.120 bilioni ambapo utakwenda kusimamia utoaji wa huduma za maji safi na salama, usimamizi wa taka ngumu, kuboresha mipango miji pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kuibua fursa za kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shughuli kuu tano zimeshatekelezwa na Shirika la ENABEL katika kuimarisha mfumo wa watoa huduma zisizo za kifedha, kuimarisha mfumo wa watoa huduma za kifedha, kuimarisha namna ya kujifunza, kuratibu na majadiliano kwa wadau mbali mbali wanaohusika na mradi, kuimarisha mfumo wa Mamlaka ya Amali pamoja na kuimarisha mfumo wa kidijitali wa ujasiriamali na kukuza stadi za ujasiriamali.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Baadhi ya Sheria ya VAT kwa upande wa Zanzibar ni changamoto hususan kwa Taasisi zisizo za Kiserikali NGOs hali inayopelekea kutokupata misamaha kwa vifaa ambayo vitatumika katika utekelezaji wa Mradi.

ii. Kukosekana kwa mashirikiano na baadhi ya wadau.

iii. Kuingiliana kwa Mipango ya Kisekta na Mipango ya Mradi katika Wizara zinazohusika na utekelezaji wa Mradi huo.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri kuangaliwa vyema Sheria ya VAT hasa kwa kuzingatia umuhimu wa mahitaji ya vifaa ambavyo vitatumika katika Miradi inayotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali ili kuweza kukamilika kwa wakati na kuleta tija

iliyokusudiwa.

ii. Ili kuhakikisha malengo ya Mradi yanafikiwa kwa walengwa, Kamati inashauri kuendeleza mashirikiano kwa baadhi ya wadau wa utekelezaji wa Mradi huo pamoja na kuwashirikisha wazawa ili kufahamu kwa kina malengo ya mradi huo.

iii. Kamati inashauri kwa upande wa Mashirika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kwa kila kipindi cha robo ya utekelezaji ili kuleta uwazi na kutokuingiliana kwa Mipango ya Kisekta katika Wizara na Mipango ya Mradi.

## SEHEMU YA TANO

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Kimuundo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) inajumuisha mafungu makuu saba (7) ambayo ni Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango F01, Mfuko Mkuu wa Serikali F02, Tume ya Mipango F03, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali F04, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali F05, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali F06 na Ofisi ya Msajili wa Hazina F07. Mafungu hayo yanaundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (7) na Ofisi tano (5) za Pemba.

Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ni Mamlaka ya

Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA), Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT).

Majukumu ya Msingi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ni Kusimamia mapato ya Serikali kutoka katika vyanzo mbali mbali, Kusimamia mali za Serikali kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoshaji wa mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali katika Mashirika ya umma, Kusimamia Fedha za Umma na Shughuli za Uhasibu Serikalini, Kusimamia Deni la Taifa, Kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Fedha inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii, Soko la Hisa na Mitaji, na Kusimamia Teknolojia ya habari na Mawasiliano kuhusiana na mapato, matumizi na Malipo ya Serikali.

## Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) yanajumuisha mafungu manne (4) ambayo ni Fungu F01 Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Fungu F04 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Fungu F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, na Fungu F07 Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ilikadiriwa kukusanya TZS 2,768 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 11 ya makadirio ya kukusanya TZS 2,498 bilioni ya mwaka wa fedha 2022/2023. Mapato halisi ni TZS 2,765.846 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 100 ya makadirio. Mapato hayo yanajumuisha mapato ya Fungu F01 TZS 1,940.935 bilioni, Fungu F04 TZS 103 milioni, na Fungu F05 TZS 824.807 bilioni.

Kwa upande wa kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Ofisi ya Rais - Fedha na

Mipango (ORFM) imekusanya TZS 1,283.59 bilioni sawa na asilimia 65 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,963.13 bilioni. Mapato haya ya TZS 1,283.59 bilioni yanajumuisha mapato ya Fungu F01 TZS 916.241 bilioni, Fungu F04 TZS 41.25 milioni, Fungu F05 TZS 359.36 bilioni na Fungu F07 TZS 7.95 bilioni.

**Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025**

Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) yanajumuisha mafungu saba (7) ambayo ni Fungu F01 Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM), Fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu F03 Tume ya Mipango, Fungu F04 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Fungu F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu F06 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, na Fungu F07 Ofisi ya Msajili Hazina.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 682.996 bilioni ambapo hadi kufikia Juni 2024 ilifanikiwa kutumia TZS 509.518 bilioni sawa na asilimia 75 ya makadirio. Matumizi hayo yanajumuisha matumizi ya Fungu F01 TZS 197.463 bilioni, Fungu F02 TZS 283.517 bilioni, Fungu F03 TZS 5.98 bilioni, Fungu F04 TZS 5.855 bilioni, Fungu F05 TZS 12.012 bilioni, na Fungu F06 TZS 4.687 bilioni.

Kwa upande wa kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) imetumia TZS 262.84 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya TZS 318.49 bilioni ya kipindi cha tathmini. Matumizi hayo yanajumuisha matumizi ya Fungu F01 TZS 32.98 bilioni, Fungu F02 TZS 210.47 bilioni, Fungu F03 TZS 4.59 bilioni, Fungu F04 TZS 3.93 bilioni, Fungu F05 TZS 6.70 bilioni, Fungu F06 TZS 2.42 bilioni, na Fungu F07 TZS 1.74 bilioni.

**Tathmini ya Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, matumizi ya kazi za maendeleo kwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) yalikuwa ni TZS 53.073 bilioni sawa na asilimia 10

ya jumla TZS 509.518 bilioni ambazo zimetumika kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo katika mchanganuo ufuatao:

i. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali: Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imetumia TZS 9.41 bilioni sawa na asilimia 49 ya makadirio ya TZS 74.12 bilioni kwa mwaka.
ii. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG Z): Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imetumia TZS 17.6 bilioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya TZS 22.8 bilioni kwa mwaka.
iii. Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM): Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imetumia TZS 726.206 milioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya TZS 1.72 bilioni kwa mwaka.
iv. Programu ya Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar: Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imetumia TZS 1.91 bilioni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya TZS 2.5 bilioni kwa mwaka.
v. Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo: Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu umetumia TZS 300 milioni sawa na asilimia 20 ya makadirio ya TZS 1.5 bilioni kwa mwaka.
vi. Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa: Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu umetumia TZS 190 milioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya TZS 2.0 bilioni kwa mwaka.
vii. Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP): Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imetumia TZS 3.01 bilioni sawa na asilimia 68 ya makadirio ya TZS 4.4 bilioni kwa mwaka.

Kwa upande wa kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, matumizi ya kazi za maendeleo kwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) yalikuwa ni TZS 17.41 bilioni sawa na asilimia 7 ya jumla TZS 262.84 bilioni zilizotumika kugharamia Programu na Miradi ya Maendeleo katika mchanganuo ufuatao:

i. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali: Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Programu hii imetumia TZS 7.32 bilioni sawa na asilimia 34 ya makadirio ya TZS 20.98 bilioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 6 ya makadirio ya TZS 113.98 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.
ii. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG Z): Katika kipindi cha Julai -

Disemba 2024/2025, Programu Big Z imetumia TZS 4.53 bilioni sawa na asilimia 21 ya makadirio ya TZS 21.56 bilioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 14 ya makadirio ya TZS 32 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

iii. Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (IS-PDRM): Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, TZS 190.27 milioni zimetumika sawa na asilimia 48 ya makadirio ya TZS 393.44 milioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 14 ya makadirio ya TZS 1.065 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

iv. Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP–VI): Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Programu imetumia TZS 1.044 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya TZS 2.50 bilioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 23 ya makadirio ya TZS 4.458 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

v. Programu ya Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar: Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, program hii imetumia jumla ya TZS 1.45 bilioni sawa na asilimia 54 ya makadirio ya TZS 2.667 bilioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 48 ya makadirio ya TZS 3.00 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

vi. Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, ZDV 2050, SDGs na African Agenda 2063): Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, jumla ya TZS 439.60 milioni zimetumika sawa na asilimia 83 ya makadirio ya TZS 531.07 milioni katika kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 19 ya makadirio ya TZS 2.28 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

vii. Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP): Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, mpango huu umetumia jumla ya TZS 2.38 bilioni zimetumika sawa na asilimia 52 ya makadirio ya kipindi cha tathmini na sawa na asilimia 27 ya makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

viii. Programu ya Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia: Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Program hii imetumia jumla ya TZS 74.1 millioni sawa na asilimia 43 ya makadirio ya TZS 171 milioni kwa kipindi cha tathmini.

**Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Kwa**

**Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imefanikiwa kukusanya jumla ya TZS 718.760 bilioni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya TZS 675.601 bilioni ya kwa mwaka. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 27 ukilinganisha na TZS 565.89 bilioni zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2023/2024 ZRA ilitumia jumla ya TZS 22.93 bilioni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya kutumia TZS 28.56 bilioni. Fedha hizo zimejumuisha TZS 4.113 bilioni ambazo zimetumika kwa kazi za maendeleo na TZS 18.817 bilioni kwa kazi za kawaida.

Kwa kiasi kikubwa ZRA iliweza kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu, kuimarika kwa uhusiano wa ZRA na wafanyabiashara, kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, kuongezeka kwa wigo wa walipakodi kwa kusajili walipakodi wapya, kuongezeka kwa ufanisi wa Mamlaka, na kuimarika kwa ushirikiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii, Ofisi ya Uhamiaji pamoja na taasisi zote za Serikali.

Kwa upande wa kipindi cha Julai – Disemba 2024/2025, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imeweza kukusanya jumla ya TZS 429.03 bilioni sawa na asilimia 103 ya makadirio ya TZS 418.50 bilioni ya kipindi cha tathmini. Kwa kulinganisha na makusanyo ya TZS. 351.769 bilioni ya kipindi kama hicho mwaka 2023/2024, kuna ongezeko la TZS 77.269 bilioni sawa na asilimia 21.96. Matumizi ya ZRA katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025 ni TZS 13.847 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya kutumia TZS 14.609 bilioni. Fedha hizo zimejumuisha TZS 2.364 bilioni ambazo zimetumika kwa kazi za maendeleo na TZS 11.483 bilioni kwa kazi za kawaida.

Uvukaji wa malengo ya makusanyo umechagiwa na mambo mbali mbali kama vile kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, kuimarika kwa mashirikiano kati ya ZRA na wafanyabiashara, kuimarika kwa uzuwiaji wa Kodi (Withholding Tax), kuongezeka kwa uwajibikaji wa hiari kwa

walipakodi, kuwepo kwa Ofisi za Mikoa, na kuimarika kwa ushirikiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii, Ofisi ya Uhamiaji pamoja na taasisi zote za Serikali.

### Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar katika mwaka wa fedha 2023/2024 imefanikiwa kukusanya TZS 508.077 bilioni ya makadirio ya kukusanya TZS 520.640 bilioni sawa na asilimia 98 ya lengo. Aidha, katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, TRA - Zanzibar imekusanya TZS 321.58 bilioni dhidi ya makadirio ya kukusanya TZS 300.94 bilioni hii ni sawa na ufanisi wa asilimia 107 ya lengo.

TRA Zanzibar imeonyesha ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato. Hii ni dalili ya utendaji mzuri wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi bora wa mapato hayo. Mafanikio ya TRA Zanzibar yamechangizwa kwa kiasi kikubwa na na mikakati mbalimbali madhubuti, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa miradi ya kimkakati katika ulipaji wa Kodi ya Zuio, utoaji wa elimu na mafunzo ya kodi kwa wadau na umma, kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa uondoshaji wa shehena maeneo ya Forodha (Tanzania Electronic Single Window System) ili kuharakisha uondoshaji wa shehena bandarini, kuanzishwa kwa ofisi ya Wilaya Wete, uboreshaji wa mifumo ya forodha na kodi za ndani, ufunguzi wa vituo vya kikodi (tax centre), na ununuzi wa scanner mpya za kisasa. Mikakati hii imewezesha TRA - Zanzibar kufikia malengo yake na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya Zanzibar.

### Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) katika mwaka wa fedha 2023/2024 ilitarajia kukusanya jumla ya TZS 178.531 bilioni na ikafanikiwa kukusanya TZS 182.229 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 102 ya lengo. Aidha, matumizi halisi ya PBZ kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yalikuwa TZS 101.77 bilioni sawa asilimia 93 makadirio ya kutumia TZS 108.912 bilioni. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, PBZ ilifanikiwa kupata faida ya jumla TZS 80.4 bilioni ukilinganisha na kiwango kilichokadiriwa cha TZS 69.6 bilioni ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 16.

Kwa upande wa kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, PBZ ilikusanya jumla ya TZS 110.04 bilioni sawa na asilimia 105 ya lengo la kukusanya TZS 116.23 bilioni. Aidha, PBZ imetumia TZS 67.20 bilioni sawa asilimia 109 ya lengo la kutumia TZS 61.61

bilioni. Kwa upande wa faida kipindi hichi cha Julai - Disemba 2024/2025, taarifa zinaonesha PBZ imeendelea kufanikiwa kupata faida ya jumla ya TZS 49.03 bilioni ukilinganisha na kiwango kilichokadiriwa cha TZS 48.43 bilioni ikiwa ni sawa na ufanisi wa asilimia 101.

### Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 750 milioni, na kufanikiwa kukusanya TZS 510.812 milioni ambazo ni sawa na asilimia 68 ya makadirio. Mapato hayo yametokana na ada ya usajili wa watoa huduma, ada ya mafunzo kwa wadau wa ununuzi, ada za nyaraka ya zabuni na ada ya matangazo. Aidha, makadirio ya matumizi ya ZPPDA yalikuwa ni TZS 2.617 bilioni na kufanikiwa kutumia TZS 2.109 bilioni sawa na asilimia 81.

Kwa kipindi cha miezi sita (6) cha mwaka wa fedha 2024/2025, Mapato ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) yalikadiriwa kuwa jumla ya TZS 515 milioni. Mapato halisi yamefikia TZS 333 milioni sawa na asilimia 65 ya makadirio. Mapato hayo yametokana na ada ya usajili wa watoa huduma, ada ya mafunzo kwa wadau wa ununuzi, ada ya nyaraka ya zabuni na ada ya matangazo. Aidha, ZPPDA ilipanga kutumia TZS 1.230 bilioni na kufanikiwa kutumia TZS 1.253 bilioni sawa na asilimia 102.

### Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) lilipanga kukusanya jumla ya TZS 49.5 bilioni, lakini lilifanikiwa kukusanya TZS 41.6 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 84 ya makadirio ya mwaka. Mapato haya yalitokana na malipo ya bima (premiums), uwekezaji, na huduma nyengine za kifedha. Kwa upande wa matumizi, ZIC ilitumia jumla ya TZS 23.8 bilioni. Kati ya fedha, TZS 8.9 bilioni zilitumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa ofisi (Management Expenses), ambayo ni sawa na asilimia 68 ya makadirio, TZS 10.8 bilioni zimetumika kulipa madai mbalimbali ya wateja wa Shirika waliopata ajali, na TZS 4.1 bilioni zimetumika

kulipa ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara kwa niaba ya ZIC.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) limefanikiwa kukusanya kiasi cha TZS 54 bilioni ya mauzo ya Bima ambayo ni sawa na asilimia 143 ya makadirio ya kukusanya TZS 37.7 bilioni katika kipindi cha tathmini. Aidha, matumizi ya Shirika kwa kipindi cha Julai - Disemba 2024 yamegawanyika kama ifuatavyo: kwanza, TZS 4.8 bilioni zilitumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa ofisi (Management Expenses), ambayo ni sawa na asilimia 77.2 ya makadirio ya matumizi katika kipindi hicho cha tathmini ambayo yalikuwa TZS 6.2 bilioni. Pili, TZS 3.4 bilioni zimetumika kulipa madai mbalimbali ya wateja wa Shirika waliopata ajali.

### Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) uliweza kufanikisha mafanikio makubwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa upande wa mapato, ZSSF ilipanga kukusanya jumla ya TZS 231.9 bilioni, ambapo ilifanikiwa kukusanya TZS 380.59 bilioni, ikizidi makadirio kwa asilimia 64. Hii inaonyesha ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato. Kuhusu matumizi, ZSSF ilitumia jumla ya TZS 321.69 bilioni, ikifika asilimia 90 ya bajeti iliyopangwa ya TZS 358.34 bilioni.

Katika kipindi cha Julai - Desemba 2023/2024, ZSSF ilikusanya jumla ya TZS 134.61 bilioni, ikiwa ni sawa asilimia 83 ya lengo la kukusanya TZS 161.94 bilioni. Kwa upande wa matumizi ya ZSSF katika kipindi hicho yalifikia TZS 195.20 bilioni, ikiwa ni asilimia 73 ya bajeti iliyopangwa ya TZS 267.02 bilioni.

### Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024/2025, Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) imepokea jumla ya TZS 553.33 milioni kama ruzuku kutoka Serikalini, ikiwa ni asilimia 71.4 ya makadirio ya TZS 775.00 milioni. Kati ya fedha hizo, TZS 453.33 milioni zimetengwa kwa matumizi mbalimbali, huku TZS 135.00 milioni zikielekezwa kwenye malipo ya mishahara. Aidha, katika mapato ya ndani, ZIAT imekusanya TZS 19.76 milioni, sawa na asilimia 26 ya lengo la TZS 76.0 milioni.

Kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai - Disemba 2024, ZIAAT imetumia jumla ya TZS 423.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 74 ya makisio ya kutumia TZS 572.0 milioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Baadhi ya taasisi za Serikali zinashindwa kulipia malipo ya bima kwa wakati licha ya kuwahi kuchukuwa ankara za malipo hayo na taasisi nyengine za Serikali kutokata kabisa bima za gari na mali zao.
ii. Kuwepo kwa ushindani mkubwa katika soko la bima Tanzania unaosababishwa na kuongezeka kwa kampuni zinazotoa huduma za bima na vile vile kuruhusiwa kwa benki kutoa huduma za bima.
iii. Kuwepo kwa uhaba wa fedha kwa ajili ya kutekeleza programu na miradi ya maendeleo.
iv. Kutokuwa tayari kufuata Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa baadhi ya waajiri na waajiriwa hali inayopelekea kutokuwajibika katika ufanyaji wa usajili na uchangiaji.
v. Kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hawatumii mashine za kutoa risiti za kielektroniki na pia kuwepo kwa wananchi wengi ambao hawana muamko wa kudai risiti. Hii inasababisha upotevu wa mapato ya kodi.
vi. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kukabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo, ambayo inazuia benki hiyo kuingia katika ushindani wa kutoa mikopo zaidi na kuongeza matawi katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango (ORFM) kwa juhudi zake katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, inaisisitiza kuweka mpango madhubuti ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili miradi ya maendeleo unakuwa wa kutosha. Hii inaweza kufanikiwa kufanya tathmini ya kina ya miradi, kuweka vipaumbele vinavyoweza kutekelezeka, kushirikiana na sekta binafsi kupitia ushirikiano katika miradi ya maendeleo (PPP), na kutafuta vyanzo mbadala vya fedha. Aidha, kuwepo uimarishaji wa mipango ya matumizi na ufuatiliaji wa miradi ili kuhakikisha fedha zilizopatikana zinatumika kwa ufanisi na miradi inakamilika kwa wakati.

ii. Kamati inaishauri ZRA na TRA Zanzibar kuongeza usajili wa walipa kodi wapya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.
iii. Kamati inaishauri ZRA kuendelea kuimarisha mahusiano na walipa kodi na kusisitiza matumizi ya mashine za elektroniki za kutoa risiti kwa wafanyabiashara na kuendelea kutoa elimu zaidi.
iv. Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa kodi ikiwa ni pamoja na kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili nayo iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi.
v. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taasisi zote nunuzi zinafanya manunuzi kupitia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (eProcurement).
vi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuongeza wigo wa kodi kwa kuimarisha sekta binafsi.
vii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ukusanyaji wa mapato hususan yasiyo ya kodi yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika hili, Serikali ihakikishe mifumo ya ukusanya wa mapato ya taasisi zote za umma inaunganishwa katika mfumo wa ukusanyaji mapato (ZanMalipo).
viii. Kamati inaishauri Serikali kuelekeza fedha katika maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya.
ix. Kamati inaishauri Shirika la Bima (ZIC) kuandaa mkakati maalum wa kufuatilia taasisi za Serikali zinazochelewa kufanya malipo ya bima na kuhakikisha kuwa malipo hayo yanafanywa kwa wakati.
x. Kamati inaushauri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuimarisha uelimishaji na uhamasishaji kupitia kampeni, warsha, na vyombo vya habari ili kuongeza uelewa kuhusu faida za hifadhi ya jamii kama vile Mafao ya Uzeeni, Mafao ya Ulemavu, Mafao ya Uzazi, Mafao ya Kuumia Kazini pamoja na Mafao ya Upotevu wa Ajira. Aidha, ni muhimu kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na utekelezaji kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuwaajibisha waajiri wanaokaidi kuwasajili na kutoa michango ya wafanyakazi wao. Sambamba na hayo, ZSSF inapaswa kurahisisha mchakato mzima wa usajili na uchangiaji kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, kushirikisha na wadau wengine kama vile vyama vya wafanyakazi na sekta binafsi, na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma ili

kuongeza imani ya wananchi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

xi. Kamati inaishauri Serikali kuanza kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo.

xii. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia za kuongeza mtaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kupitia ubia na mwekezaji wa kimkakati na pia kukuza mtaji kupitia mapato ya ndani ya benki. Hii itasaidia benki kuingia kwenye ushindani wa kutoa mikopo zaidi na kuongeza matawi katika mikoa mbalimbali na kuweza kuwa benki kubwa Tanzania kama vile zilivyo CRDB, NMB na NBC.

## SEHEMU YA SITA

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

### Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA)

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) imeanzishwa kwa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2011. Majukumu makuu ya Mamlaka ni kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege. Miongoni mwa vyanzo vya mapato vya Mamlaka ni pamoja na ada ya utuaji na uegeshaji wa ndege, kodi ya majengo, ada ya biashara, tozo ya matangazo, uegeshaji wa magari, mapato ya ukumbi wa watu mashuhuri, ada ya vitambulisho, ada ya usalama wa kiwanja, na mapato mengineyo.

Katika kipindi Julai – Septemba 2024/2025, Mamlaka ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 14.412 bilioni. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kukusanya jumla ya TZS 11.789 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya kipindi hicho. Kwa upande wa matumizi, Mamlaka imekadiria kutumia TZS 13.484 bilioni ambapo matumizi halisi ni TZS 9.840 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, makadirio ya mapato ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) yalikuwa TZS 42.183 bilioni ambapo mapato halisi TZS 40.210 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi, Mamlaka imekadiria kutumia TZS 38.897 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 21.940 bilioni ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na TZS 16.957 bilioni ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2024, Mamlaka imetumia jumla ya TZS 32.498 bilioni sawa na asilimia 84 ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) inatekeleza miradi mitatu (3) kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Abiria la Terminal 1: Mradi huu umekadiriwa kutumia jumla ya USD 6.127 milioni ambazo USD 300,000 ni kwa ajili ya kazi za ushauri elekezi na USD 5.827 milioni kwa ajili ya ujenzi. Hadi kufikia Septemba 2024, mradi huu ulishatumia jumla ya USD 2.262 milioni na ujenzi umefikia asilimia 45%. Mradi huu umeanza tarehe 15/04/2024 na ulitegemewa kukamilika tarehe 15/02/2025.

ii. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria la Terminal 2: Mradi huu umekadiriwa kutumia jumla ya USD 34 milioni ambazo USD 2 milioni ni kwa ajili ya kazi za ushauri elekezi na USD 32 milioni kwa ajili ya ujenzi. Hadi kufikia Septemba 2024, mradi huu ulishatumia jumla ya USD 12.744 milioni na umefikia asilimia 38. Kati ya fedha hizo, USD 10.299 milioni zimelipwa kupitia ZAA na USD 2.445 milioni kupitia Serikali kuu. Mradi umeanza tarehe 31/12/2023 na unategemewa kukamilika tarehe 30/10/2025.

iii. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Biashara Terminal 3: Mamlaka kwa kushirikiana na muwekezaji (East Africa Developer Limited) inajenga Jengo la ghorofa 3 (G plus 3) ambalo litakuwa na maeneo ya ofisi, mabenki na mikahawa. Mkandarasi wa mradi huu ni Kampuni ya Eastim Enterprises Company Limited. Mradi huu umeanza rasmi tarehe 17/4/2024 na unategemewa kukamilika tarehe 16/11/2025. Hadi kufikia Oktoba 2024, mradi umefikia asilimia 28.

## Changamoto Zilizobainika

i. Uchakavu wa miundombinu katika Jengo la Abiria Terminal 2.
ii. Uchakavu wa vifaa vya ulinzi na usalama.
iii. Uhaba wa wafanyakazi na uwepo wa wafanyakazi wa mkataba ambao bado hawajaajiriwa.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Ili kushughulikia uchakavu wa miundombinu, ni muhimu kufanya tathmini na kuandaa mpango wa ukarabati unaohusisha vifaa, mifumo ya umeme na maji, na uboreshaji wa mazingira ya jengo. Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka inapaswa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya ukarabati huo na kuimarisha miundombinu katika viwanja vya ndege, ikiwemo mifumo ya umeme, mifumo ya maji, viti vya abiria, na maeneo ya wageni mashuhuri. Pia, kuwezesha ufungaji wa vifaa vya kisasa kama lifti, eskaleta, na mifumo ya viyoyozi inayoendana na mazingira viwanja vyetu sambamba na kuongeza ufanisi wa huduma zake.

ii. Kuhusiana na changamoto ya uchakavu wa vifaa vya ulinzi na usalama inaweza kushughulikiwa kwa kuwezesha ununuzi wa vifaa vipya vya kisasa ambavyo vinakidhi viwango vya kimataifa vya usalama wa anga. Mamlaka husika inapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaa vya ulinzi kama kamera za CCTV, mashine za skana za mizigo, na vifaa vya ukaguzi wa abiria ili kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo. Pia, kufanya mafunzo ya mara kwa mara

kwa maafisa wa usalama kuhusu matumizi ya teknolojia mpya na mbinu bora za kiusalama kutasaidia kuimarisha usalama wa eneo hilo.

ii. Ili kutatua changamoto ya uhaba wa wafanyakazi na uwepo wa wafanyakazi wa mkataba ambao bado hawajaajiriwa, Kamati inaishauri Mamlaka iombe kibali cha ajira na kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi wa mkataba wenye sifa zinazohitajika ili kuimarisha uthabiti wa rasilimali watu. Pia, Serikali inaweza kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi na kuongeza watendaji kwa kadri inavyostahiki ili kupunguza mzigo wa kazi kwa wafanyakazi waliopo. Njia nyingine ni kushirikiana na taasisi za mafunzo ya usafiri wa anga ili kuajiri wahitimu wapya kupitia programu za mafunzo kazini (internship) na kuwapa nafasi za kudumu baada ya kuthibitishwa kwa ufanisi wao.

## Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Maji Nam.4 ya Mwaka 2006 ambayo inatekeleza jukumu la msingi la kusambaza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar na kusimamia rasilimali ya maji.

Katika kipindi cha Julai - Septemba 2024/2025, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imepanga kukusanya na kutumia TZS 42.287 bilioni kwa kazi za maendeleo ambapo hadi kufikia Septemba 2024 jumla TZS 3.837 bilioni zimetumika. Aidha, ZAWA ilipanga kukusanya TZS 5.28 bilioni ikiwa TZS 2.996 bilioni ni kutokana na ada za huduma ya maji na TZS 2.284 bilioni ni ruzuku ya mshahara kutoka Serikalini. Hadi kufikia Septemba 2024 jumla ya TZS 2.048 bilioni zimekusanywa ikiwa TZS 914,527 milioni ni mapato ya ada za huduma ya maji na TZS 1.964 bilioni ni ruzuku ya Mshahara kutoka Serikalini.

Kwa upande wa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024/2025, ZAWA imetekeleza miradi na programu mbali mbali kama ifuatavyo:

i. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar
ii. Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar
iii. Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Miundombinu ya Maji Mjini
iv. Programu ya UNICEF
v. Mradi wa Uimarishaji Miundombinu ya Maji

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilipanga kukusanya kiasi cha TZS 89.764 bilioni ambapo matumizi halisi ni TZS 53.002 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 59.00 ya makadirio. Kwa upande wa matumizi, ZAWA ilipanga kutumia TZS 89.764 bilioni kati ya fedha hizo TZS 67.030 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na TZS 22.733 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida. Hadi kufikia Juni 2024 jumla ya TZS 53.097 bilioni zimetumika ikiwa TZS 41.005 bilioni kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo na malipo ya madeni ya watoa huduma za vifaa vya maji na TZS 12.091 bilioni kwa kazi za kawaida katika uimarishaji wa miundombinu ya maji mafunzo kwa wafanyakazi, mishahara na uendeshaji wa Ofisi.

Ukiangalia jumla ya kiwango cha mapato na matumizi utabaini kuwepo kwa tofauti ya TZS 94.611 milioni. Fedha hizi, zilitakiwa kulipwa fidia katika mwaka wa fedha 2022/2023 na badala yake malipo yake yakafanyika mwaka wa fedha 2023/2024.
Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ZAWA imetekeleza miradi mbali mbali kama ifuatavyo:

i. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi
ii. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar
iii. Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar
iv. Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar (SMZ)
v. Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar
vi. Mradi wa Usimamizi wa Maji (UNICEF)

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa kupanda na kushuka kwa umeme mara kwa mara kunakopelekea kutokezea hitilafu za kuungua pampu na vifaa katika visima,
ii. Kuwepo kwa uchakavu wa miundombinu ya maji hususan bomba za Asbestos cement (AC) na uPVC,
iii. Kukosekana kwa hatimiliki katika maeneo ya vyanzo vya maji,
iv. Kuwepo kwa uvamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na hujuma za miundombinu ya maji

v. Kuwepo kwa uharibifu wa mitandao ya maji unaosababishwa na ujenzi wa miundombinu ya barabara unaoendelea katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

vi. Kuwepo kwa vitendo vya wizi wa nyaya katika maeneo ya vibanda vya kuendeshea pampu za maji,

vii. Kuwepo kwa vitendo vya wizi wa mita za maji katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuweka miundombinu ya barabara kuelekea katika miradi mikubwa ya maji kwani kutasaidia kufikika kwa urahisi hasa wakati inapotekezea dharura kama vile hitilafu za umeme. Pia itasaidia watendaji wanaohudumu katika maeneo hayo kama vile walinzi na wahandisi kufika eneo la mradi kwa urahisi na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa wakati na kwa ufanisi.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuweka bajeti maalum kwa ajili ya kuiwezesha ZAWA kufanya marekebisho ya miundombinu ya maji iliyoharibika.
iii. Kamati inaishauri ZAWA kufanya marekesho ya haraka katika miundombinu ya maji kwa kubadilisha mabomba chakavu na kulaza mapya ili kuweza kuhuwisha huduma ya maji na kuwa endelevu katika maeneo ya Unguja na Pemba.
iv. Kamati inaishauri ZAWA kuhifadhi maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yake kwa kujenga uzio, kutafuta hatimiliki na kuweka ulinzi.
v. Kamati inaishauri ZAWA kufunga vifaa maalum vya kudhibiti ongezeko la umeme ili kuepusha uunguaji wa pampu na vifaa vya umeme mara kwa mara.
vi. Kamati inaipongeza sana ZAWA kwa kuimarisha miundombinu ya maji kama vile ujenzi wa matangi na uchimbaji wa visima kwa kiasi kikubwa, Kamati inashauri ZAWA sasa ielekeze nguvu kubwa katika usambazaji wa maji kwa wananchi ili kufikia. Bila ya maji kufika wananchi, juhudi zote hizi inakuwa hazijafikia lengo lililokusudiwa.

## Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ)

Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) imeanzishwa Mwaka 2024 kwa Sheria Namba 1 ya mwaka 2024. Mamlaka ina majukumu ya kuandaa na kusimamia sera,

kanuni, na mipango ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma. Aidha, Mamlaka inashauri Serikali kuhusu matumizi bora ya TEHAMA, kuendeleza matumizi yake katika taasisi za umma kwa ufanisi na uthabiti, na kuwezesha ubadilishaji wa taarifa kati ya taasisi za Serikali, sekta binafsi, na wananchi. Pia, Mamlaka inatoa miongozo na kufanya tathmini ya ubora wa mifumo ya TEHAMA, kuhakikisha vifaa vinakidhi viwango, na kusimamia utekelezaji wa Sera ya usalama wa TEHAMA katika utumishi wa umma.

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2024, Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya TZS 1.045 bilioni ambapo TZS 384.2 milioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya mishahara na TZS 660.5 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi cha fedha kilichoingizwa ni TZS 800.6 milioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya hizo, TZS 410.1 milioni asilimia 109 ya zilitumika kwa mishahara, na TZS 390.5 milioni sawa na asilimia 59.12 zilitumika kwa matumizi mengineyo.

Kwa upande wa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilikadiria kutumia jumla ya TZS 3.209 bilioni, ambapo TZS 1.250 bilioni zilipangwa kwa mishahara na TZS 1.959 bilioni kwa matumizi ya kawaida. Hadi 30 Juni 2024, jumla ya TZS 2.866 bilioni sawa na asilimia 89 ya makadirio zilipatikana. Kati ya hizo, TZS 1.451 bilioni sawa na asilimia 116 ya makadirio ilitumika kwa mishahara, na TZS 1.415 bilioni sawa na asilimia 72 ya makadirio ilitumika kwa matumizi ya kawaida, pamoja na fedha zilizoingizwa kupitia uratibu wa mifumo ya ZanVibali, ZanMalipo, na BAMAS.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kuwepo kwa ufinyu wa nafasi katika ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ) ambapo imepelekea watendaji wengi kukusanyika katika eneo dogo. Hali hii inapelekea kupunguza ufanisi wa kazi.
ii. Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ) inakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi.
iii. Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ) inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi. Hii inapunguza ufanisi wa kazi na utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kutokana na kuwepo kwa vitendo vya udukuzi katika mifumo ya kiteknolojia ya

kisasa ya TEHAMA, Kamati inaishauri eGAZ kuweka mipango madhubuti ya kulinda usalama wa mifumo ya Serikali hususan ya mapato. Aidha, Kamati inaishauri eGAZ kuishauri Serikali kwa karibu kuhusiana na suala hili la usalama wa mifumo.

ii. Kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa eGAZ na hatimae kufanikisha kuimarisha mfumo mzima wa kidijitali wa Serikali, Kamati inaishauri Serikali kulipa suala la ujenzi wa jengo la ofisi na upatikaji wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi ni muhimu sana kupewa kipaumbele kwani eGAZ ni taasisi inayotegemewa katika uendeshaji wa Serikali kwa njia ya mtandao. Katika nchi zote duniani, Mamlaka zinazohusiana na Serikali Mtandao ni miongoni mwa taaasisi zinazochukuliwa kwa uzito mkubwa kutokana na mchango wake kwa nchi kwani Serikali za kisasa zinategemea mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji wake.

iii. Ili kutatua changamoto ya uhaba wa wafanyakazi katika Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ), Serikali inapaswa kuweka mpango maalum wa kuajiri watumishi wapya kulingana na mahitaji ya mamlaka na kuhakikisha kunakuwepo uwiano sahihi wa majukumu. Pia, Mamlaka iimarishe mifumo ya mafunzo na kuongeza ufanisi wa wafanyakazi waliopo kwa kuwapa ujuzi wa ziada kupitia mafunzo ya mfupi na mrefu. Mbinu nyingine ni kutumia wataalamu wa muda (consultants) na programu za mafunzo ya kazi (internship) kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ambao wanaweza kusaidia kupunguza mzigo wa kazi kwa watendaji wa kudumu, na huku wakichangia katika uendelevu wa taasisi.

## Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)

Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) lilianzishwa rasmi mwezi Julai 1997 chini ya Sheria Nambari 1 ya mwaka 1997. Kwa sasa, Shirika lina wafanyakazi 198 baada ya wafanyakazi 385 kuhamishiwa kwa mwekezaji wa Bandari ya Malindi, ZMT. Lengo kuu la Shirika ni kuhudumia Bandari zote za Unguja na Pemba.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) kwa kushirikiana na wawekezaji wa Bandari ya Malindi, Fumba, na Mkoani, lilifanikisha kutoa huduma mbalimbali. Kwa meli za kigeni, lilihudumia safari 116 kati ya 120 zilizopangwa (97%). Kwa meli za ndani, safari 4,017 kati ya 4,150 (97%) zilifanyiwa

huduma, na kwa majahazi, safari 3,337 kati ya 3,500 (95%) zilikamilika. Kuhusu mizigo, Shirika lilihudumia tani 563,866.57 za mizigo mchanganyiko ya meli (75% ya makadirio) na tani 139,821.5 za mizigo ya majahazi (111%, ikiwa ni ongezeko la tani 13,621.5). Kwa mafuta ya kuwasha, lita 130,285,082 (93%) zilihudumiwa kati ya lita 140,000,000 zilizopangwa. Kwa makontena, jumla ya makontena 32,992 (66%) yalihudumiwa kati ya makontena 50,000, na kwa abiria, 2,478,833 (99%) walihudumiwa kati ya abiria 2,500,000 waliotarajiwa.

Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) limeweza kutekeleza programu na miradi mbali mbali kama ifuatavyo:

i. Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari ambayo inajumuisha ujenzi wa bandari mpya tatu na ukarabati wa bandari zilizopo. Kwa Bandari ya Malindi, mradi wa bandari kavu ya Maruhubi umekamilika kwa gharama ya TZS 14.8 bilioni. Bandari ya Mangapwani inaendelea kwa awamu tatu, na mpango mkuu umekamilika. Ujenzi wa Bandari ya Mkoani unaendelea, na huduma za makontena zimeanza. Bandari ya Shumba inaendelea kwa gharama ya TZS 5.77 bilioni na imefikia 88% ya utekelezaji, huku TZS 4.09 bilioni zikitumika. Bandari ya Fumba imekamilika kwa gharama ya TZS 17.108 bilioni, ambapo TZS 15.3 bilioni zimetolewa na muwekezaji na TZS 1.808 bilioni na Serikali. Bandari ya Wete ina upembuzi yakinifu uliokamilika kwa gharama ya TZS 279.1 milioni kati ya TZS 845 milioni zilizopangwa.

ii. Mradi wa Ukarabati wa Minara, minara ya Makunduchi na Mwana wa Mwana zimekarabatiwa kwa TZS 79.9 milioni na TZS 70 milioni mtawalia, na uboreshaji wa maboya umegharimu TZS 586.9 milioni. Maboya mapya saba yamewekwa kwa TZS 398.5 milioni.
iii. Mradi wa Sea Taxi unaendelea na upembuzi yakinifu ukipangwa.
iv. Programu ya Ununuzi wa Vitendea Kazi imekamilika kwa ajili ya baji, scanner, tug, na pilot boat.
v. Programu ya TEHAMA (ePort) inaendelea na imefikia 85% ya utekelezaji kwa gharama ya TZS 14.509 bilioni.

Kwa ujumla, programu na miradi hii inalenga kuimarisha huduma za bandari na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.

Katika mwaka wa fedha 2024/25, Shirika la Bandari linatarajia kukusanya TZS 37.962 bilioni kupitia vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za meli, mizigo, mrabaha na mapato mengineyo. Katika kipindi cha Julai - Desemba 2024/2025, Shirika lilikadiria kukusanya TZS 17.344 bilioni na kufanikiwa kukusanya TZS 19.011 bilioni, ambayo ni ongezeko la TZS 1.667 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 109.6% ya makadirio.

Katika mwaka wa fedha 2024/25, Shirika la Bandari limepanga kutumia TZS 77.441 bilioni**.** Kati ya hizo, TZS 16.782 bilioni ni matumizi ya kawaida na TZS 60.658 bilioni ni kwa miradi ya maendeleo. Shirika linahitaji mkopo wa TZS 40 bilioni ili kutekeleza baadhi ya shughuli za miradi.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2024, matumizi ya kazi za kawaida yaliyopangwa ni TZS 8.742 bilioni, na hadi kufikia Disemba 2024, Shirika limefanikiwa kutumia TZS 7.076 bilioni (80.94%). Shirika pia limelipa TZS 225 milioni kwa ajili ya TRA Corporate Tax, TZS 340 milioni kama gawio kwa Serikali, na TZS 875 milioni kwa ajili ya makato ya TRA na kodi za ardhi kwa ZRA.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Shirika lilipanga kutumia TZS 6.376 bilioni katika kipindi hicho. Hadi kufikia Disemba 2024, Shirika limetumia TZS 6.080 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya kipindi hicho.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa kwa tathmini kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakaazi wa Zoni C Mangapwani.
ii. Kuwepo kwa uvamizi katika maeneo ya minara ya Shirika la Bandari.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inalishauri Shirika la Bandari kuhakikisha Mfumo wa Kielekrtoniki wa Bandari (ePort) unakuwa ni mali ya bandari kwa asilimia 100 ikiwemo programu asili (source code) ili kuwezesha kufanya marekebisho teknolojia inapobadilika au kufanya nyongeza yoyote ya kimfumo.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuyaangalia kwa karibu maslahi ya watendaji waliyohamia kwa mwekezaji wa bandari. Hatua hii itasaidia kuwaongezea morali na pia utendaji wao wa kazi.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto ya kukosekana ghala (warehouse) la kukagulia mizigo katika Bandari ya Fumba.
iv. Ili kutatua changamoto ya kuchelewa kwa tathmini na malipo ya fidia, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa tathmini kwa kuweka utaratibu mzuri na kuwepo mpango mzuri wa tathmini kuanzia hatua za awali kuepusha kutumia muda mrefu na kufanya malipo ya fidia kinyume na thamani halisi ya mali husika.
v. Ili kukabiliana na uvamizi katika maeneo ya minara ya ulinzi ya Shirika la Bandari, Kamati inaishauri kuwekwa walinzi, uzio, kamera za usalama (CCTV), na kuwepo mashirikiano ya karibu baina ya Shirika na jamii wanaoishi karibu na maeneo ya minara.

### Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar ni Shirika la Serikali lenye jukumu la kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi wa Zanzibar. Katika utekelezaji wa shughuli zake Shirika linafuata Mpango kazi na Bajeti kwa kipindi cha mwaka husika.

Shirika lilipanga kukusanya TZS 179,400,989,785.96 na makusanyo halisi ni TZS 174,984,308,205.12 sawa na asilimia 98.

Katika mwaka wa 2023/2024 ilifanya matumizi ya ununuzi wa umeme kwa Unguja na Pemba kutoka TANESCO kiasi cha TZS 96.05 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya TZS 95.37 bilioni iliyopangwa kutumika katika kipindi hicho. Aidha,TZS 1.79 bilioni zilitumika kwa ajili ya kugharamia mauzo ya umeme kwa njia ya kielectroniki sawa na ongezeko la asilimia 39 ya makadirio ya matumizi ya TZS 1.29 bilioni. Kwa upande wa matumizi ya kazi za uendeshaji kwa kipindi cha Julai - Juni 2023/2024 jumla ya TZS 35.84 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya bajeti ya TZS 37.12 bilioni zilizopangwa kutumika katika kipindi hicho.

Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, katika robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2024/2025 Shirika limekusanya jumla ya TZS 57.6 bilioni. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya umeme, mapato mengineyo pamoja na madeni ya nyuma yanayolipwa na wateja. Aidha, kwa upande wa matumizi kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2024/2025 jumla ya TZS 26.1 bilioni zimetumika kwa

ajili ya gharama za ununuzi wa umeme kwa Unguja na Pemba. Aidha, Jumla ya TZS 477 milioni zimetumika kwa ajili ya kugharamia mauzo ya umeme kwa njia ya kielectroniki sawa na asilimia 119 ya makadirio ya matumizi ya TZS 401milioni. Kwa upande wa matumizi wa kazi za uendeshaji, jumla ya TZS 6.8 bilioni zimetumika sawa na asilimia 69 ya makadirio ya bajeti ya 10 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kumekuwepo na changamoto ya baadhi ya taasisi za Serikali kulimbikiza madeni na kutolipa kwa wakati hali inayoipunguzia Shirika mapato yake. Hadi kufikia mwezi Juni 2024, Shirika linawadai wateja wake jumla ya TZS 68.41 bilioni.

ii. Kumekuwepo na vitendo vya uharibifu wa miundombinu ya usambazaji wa umeme kama vile uchimbaji wa mchanga kwenye njia kuu za umeme na wizi wa waya za shaba.

iii. Baadhi ya wateja wasiokuwa waaminifu kutumia umeme kinyume na utaratibu na kulikosesha Shirika mapato yake.

iv. Uvamizi katika njia kuu za usambazaji umeme kwa shughuli za ujenzi na ufanyaji wa biashara katika maeneo ambayo kwa mujibu wa taratibu za kiufundi ni hatari kufanyika shughuli hizo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Shirika kuendelea na juhudi zake za kukumbushia taasisi zenye madeni kulipa pamoja na kuendelea kulipia huduma ya umeme kwa wakati ili kuondokana na malimbikizo.

ii. Kamati inaishauri Shirika kuendelea kuipatia elimu jamii juu ya umuhimu wa kuitunza miundombinu ya usambazaji umeme pamoja na kujiepusha kuvamia katika njia za usambazaji umeme kwa shughuli za ujenzi na biashara ili kuondokana na hatari za maeneo hayo ambazo zinaweza kujitokeza.

### Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kilianzishwa chini ya Sheria nambari 1 ya mwaka 2003 ambacho kina jukumu la kulinda na kuhakikisha ulinzi na usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kufanya kazi za uwokozi baharini, kuzuia makosa yote yanayofanyika upande wa baharini, kulinda rasilimali za bahari, kusafirisha na kulinda misafara ya viongozi baharini pamoja na kushirikiana na jeshi la wananchi pale inapohitajika hivyo katika kuilinda Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kikosi maalum cha kuzuia magendo kiliidhinishiwa jumla ya TZS 37,620,300,000 kwa ajili ya kutekeleza programu kuu mbili mbazo ni Programu ya Ulinzi na Uokozi na Programu ya Utawala na Uwendeshaji wa huduma. Kazi ya fedha hizo, TZS 31,384,400,000 kwa ajili ya mishahara, TZS 3,735,900,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 2,500,000,000 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Juni 2024, Kikosi kiliingiziwa jumla ya TZS 38,246,738,261 sawa na asilimia 103.2 ili kutekeleza majukumu yake.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kamati imebaini kuwepo kwa bajeti ndogo ya maendeleo kuliko Bajeti ya matumizi mengineyo (OC)

ii. Uhaba wa upatikanaji wa mafuta kwa ajili ya gari za kwenda kwenye operesheni katika maeneo ya bandari bubu.

iii. Uchache wa vyombo vikubwa vya doria za baharini ambavyo vitaendana na ukubwa wa bahari ya Pemba.

iv. Kutopatikana kwa mafuta ya kutosha kwa ajili ya kuendeshea boti za doria ya magendo. Boti hizi huhitaji kiasi kikubwa cha mafuta.

v. Uchelewaji wa uchukuaji wa hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa ambao hukamatwa na KMKM.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuipangia KMKM bajeti maalum kwa ajili ya ununuzi wa rad ana ndege zisizo na rubani (drones). Hii itasaidia kuviona vyombo vilivyoko baharini hata vikiwa mbali na kuweza kuvifuatilia kwa urahisi.

ii. Kwa kuwa KMKM inakabiliwa na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya zoezi la kufuatilia na kukamata vyombo vya magendo, na kwa kuwa TRA wanayo bajeti ya kutosha ya kuzuia vitendo vya magendo lakini haina nguvu kazi ya kutekeleza hilo, Kamati inaishauri KMKM na TRA kufanya vikao vya pamoja ili kujenga mashirikiano kwa kuunda Kamati au Timu Maalum ya kukabiliana na magendo. Hatua hii inapaswa kuwekewa uzito kwa kuingia Mkataba wa Mashirikiano (MoU) baina ya KMKM na TRA. Sambamba na hilo, Kamati inazishauri KMKM na TRA kuzishirikisha taasisi

nyengine ambazo nazo zinahusika katika mapambano ya kuzuia magendo kama vile ZMA na Shirika la Bandari (ZPC).

iii. Kamati inaishauri Serikali kurudisha utoaji wa motisha kwa mtoa taarifa anayesaidia ukamataji wa mizigo ya magendo. Kwa sasa utoaji wa motisha imeondoshwa hali inayopelekea kukosekana kwa taarifa za mienendo ya vyombo vya magendo.

## Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA)

Shirika la Mawasiliano Zanzibar ni Taasisi ya Serikali iliyoanzisha kwa Sheria nambari 4 ya mwaka 2023 na kupewa jukumu la kusimamia na kuendesha mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar na kusimamia kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa kwa lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora ya mawasiliano iliyosalama na endelevu.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Shirika Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 7,000,000,000 ambapo hadi kufikia Juni 2024, Shirika limeweza kukusanya TZS 16,605,320,571 sawa na asilimia 237 za makadirio. Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TZS 15.403,688,500 ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2024 Shirika liliweza kutumia jumla ya TZS 8,793,597,976.70 sawa na asilimia 57 ya makasirio.

## Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini Shirika linakabiliwa na changamoto ya baadhi ya Taasisi za Serikali kutokulipa kwa huduma zinazotolewa na ZICTIA hali inayopelekea kukosekana kwa mapato.

ii. Kuharibika kwa njia ya mkonga wa Taifa ambako kunatokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja shughuli za kijamii zinazoendelea katika baadhi ya maeneo.

iii. Uchelewaji wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo inayo inayosimamiwa na Shirika

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inalitaka Shirika kuhakikisha linakuwa na mikakati maalum ya kuwawezesha wadaiwa wote kulipia huduma za ZICTIA ili kuliwezesha Shirika

kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

ii. Ili kuhakikisha miundombinu ya mawasiliano inabaki kuwa salama na endelevu, Kamati inalitaka Shirika kuhakikisha linafanya matengenezo ya haraka pamoja na kuwapatia elimu wananchi hususan wakati wa utekelezaji wa miradi kuhakikisha kunapatikana njia mbadala ya kuweza kuihamisha miundombinu hiyo ili iweze kutumika kwa muda mrefu.

iii. Kwa kuwa Shirika limepanga kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuhakikisha huduma za mawasiliano nchini zinakuwa za uhakika, Kamati inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha upatikanaji wa fedha za miradi inayotekelezwa na Shirika zinapatikana kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)**

Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza majukumu yake ya kawaida ikiwemo kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za maji na nishati, kuimarisha usimamizi wa upatikanaji wa bora, endelevu na salama wa huduma za maji na nishati, kuboresha uwezo wa mamlaka wa udhibiti wa huduma za maji na nishati pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

Kwa kipindi cha tathmini cha Julai hadi Septemba 2024/2025 Mmlaka ilikadiria kukusanya jumla ya TZS bilioni 13.210 ambapo hadi kufikia mwezi Disemba, Mamlaka iliweza kukusanya jumla ya TZS bilioni 13.924 sawa na asilimia 105 ya makadirio. Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ilikadiria kutumia jumla ya TZS 15,434,360,697 lakini hadi kufikia mwezi Disemba ilitumia jumla ya TZS 10,678,313,859.48.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Katika kufanya ukaguzi wa miundombinu ya kusambazia umeme katika kituo cha Ras Mnyanjani ambayo waya kutoka kituo cha Majani Mapana umeanza, Mamlaka imebaini kituo kukosa Kamera za CCTV na taa kwa ajili ya ulinzi na

usalama.

ii. Kukosekana kwa bango la tahadhari katika eneo la bahari.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri ZURA kwa kushirikiana na ZECO kufuatilia utekelezaji wa changamoto zinazojitokeza katika kituo cha Ras Mnyanjani ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi.

**Maoni na Ushauri wa Jumla**

Mwisho kabisa, wakati Kamati ya Bajeti ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2024/2025 imebaini kuwepo kwa changamoto inayoikabili taasisi nyingi za Serikali ikiwemo Wizara, Mamlaka, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tawala za Mikoa, na Idara Maalum za SMZ. Changamoto hiyo ni upatikanaji hafifu wa wa fedha za matumizi mengineyo (OC). Changamoto hii huleta athari kubwa katika utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi kutokana na taasisi hizo kukosa fedha za kugharamia mahitaji ya msingi kama vile vifaa vya ofisi, mafuta ya vyombo vya usafiri, na matengenezo ya majengo. Hivyo, hali hii hupelekea kupunguza ufanisi wa kazi, motisha kwa watumishi hali inayoweza kusababisha kushuka kwa morali ya kazi.

Kwa kuwa taarifa za mwenendo wa ukusanyaji mapato zinaonesha kuongezeka kwa mapato ya Serikali, ni matumaini ya Kamati changamoto hii ya uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC) linapatiwa ufumbuzi wa haraka kwani kwa kiasi kikubwa linakwamisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo.

## SEHEMU YA SABA

## HITIMISHO

Naomba kumalizia ripoti hii kwa kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Zubeir Ali Maulid, kwa uongozi wake makini na weledi mkubwa katika kuliongoza Baraza la Wawakilishi kwa ufanisi na uadilifu katika kutekeleza majukumu yake akisaidiwa na wasaidizi wake Mheshimiwa Naibu Spika Mgeni Hassan Juma pamoja na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Abdulla Hussein Kombo. Aidha, shukurani za dhati ziende kwa Ndg. Raya Issa Msellem Katibu wa Baraza kwa niaba ya watendaji wote wa Ofisi ya Baraza kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Nachukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi za Serikali ambao walikuja kutoa ufafanuzi mbele ya Kamati. Kamati ya Bajeti inathamini sana mashirikiano yao.

Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, pongezi za dhati ziende kwao kwa michango, maoni na ushauri wao ambao umesaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu.

Naomba kutoa hoja.